Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

## Kikao cha Sita – Tarehe 5 Februari, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 68

### Hitaji la Maji - Vwawa

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Je, ni lini wakazi wa Mji wa Vwawa zaidi ya 40,000 watapata maji ya uhakika kuliko ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshijmiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Vwawa ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi una idadi ya watu zaidi ya 50,000. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka hadi kufikia watu 56,061 ifikapo mwaka 2015. Ni kweli kuwa Mji wa Vwawa wakazi wake hawapati huduma ya maji ya uhakika. *(Makofi)*

Hii inatokana na uchakavu wa miundombinu ya maji pamoja na kupungua kwa vyanzo vya uzalishaji wa maji. Miundimbinu ya maji katika Mji wa Vwawa ilijengwa mwaka 1957 wakati huo kukiwa na idadi ya watu 5,700. Katika kipindi cha mwaka 1970 na 1990, miundombinu hiyo ilifanyiwa upanuzi au ukarabati ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji na kupunguza tatizo la uhaba wa maji kwa wakazi wa Mji wa Vwawa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012 mahitaji ya maji katika Mji wa Vwawa ulikuwa mita za ujazo 3,603 kwa siku wakati uzalishaji maji ni wastani wa mita za ujazo 1,685 sawa na 55% ya mahitaji ya siku. Miundombinu iliyowekwa ina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 1,847 kwa siku. Hata hivyo, kiwango hicho hakifikiwi kutokana na uchakavu na upungufu wa mitambo ya kusafirisha maji.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji katika Mji wa Vwawa, Serikali imeweka mipango mbalimbali ili kuondokana na hali hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Mpango wa muda mfupi wa mwaka 2012/2013. Mpango huu unalenga kuongeza uzalishaji maji kutoka mita za ujazo 1,685 zilizopo hadi kufikia mita za ujazo 2,133 kwa siku. Jumla ya shilingi milioni 60 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Mji wa Vwawa zikiwemo shilingi milioni 35 zitakazotumika kununua mashine ya kupampu maji na shilingi milioni 25 ambazo ziatumika kununua Dira za Maji (*Water Meter*) pamoja na kuendelea kuboresha miundimbinu.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imekwishatuma maombi maalum ya fedha kiasi cha shilingi milioni 162 Wizara ya Maji, kwa ajili ya ukarabati wa miundimbinu ya majai na kaugharamia ufungaji wa umeme katika mashine ya kupampu maji iliyoagizwa. Mpango huu ukikamilika utaongeza uzalishaji wa maji kwa mita za ujazo 448 kwa siku ambazo zina uwezo wa kuhudumia wananchi 6,400. Hivyo, upatikanaji wa maji utaongezeka kufikia 59.2% baada ya kukamilika kwa mpango huu.

(ii) Mpango wa Muda wa Kati mwaka 2010/2015. Katika mpango huu, Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika vyanzo vipya vilivyobainishwa. Azma ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wote katika vyanzo vipya vilivyobainishwa. Azma ya Serikali ni kuhakikisha wananchi

wote wa Mji wa Vwawa wanapata huduma za maji safi na salama kwa 80% ifikapo mwaka 2015.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza naomba tu nisikitike kwamba mji wa Vwawa ambao kama Wilaya ya Mbozi imeanza mwaka 1965 mpaka leo inatumia maji ya kutega ambayo wakati wa masika wananchi wanakunywa maji machafu na hasa wale ambao hawana uwezo wa kuchimba visima wanaishi kwa taabu sana. Naomba Serikali ilielewe hilo. Baada ya hilo, naomba nijue kwamba je, Serikali kweli imedhamiria kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Vwawa na kwa maana hiyo watapeleka sasa hizi shilingi milioni 162 ambazo zimepelekwa kama ombi maalum Wizara ya Maji?

Pili, ninaomba Serikali inihakikishie na ukizingatia sehemu ya pili ya mwisho ya mpango wa muda wa kati 2010/2015 kumaliza matatizo ya maji katika mji wa Vwawa. Je, Serikali kufikia mwaka 2015 itapeleka maji kwa 80% kama Waziri alivyotueleza?

Mimi niendelee kuifuatilia Serikali kwa ahadi hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi namwelewa Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mbeya na Mbunge wa

Mbozi Mashariki anaposema maneno haya na ninajua anasema hivyo kwa sababu anajua kwamba nimewahi kufika katika Mji huo na nikajionea mwenyewe matatizo yaliyopo pale.

Namwomba asisikitike kwa sababu anajua kabisa kwamba tumedhamiria kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Hizi shilingi milioni 62 tunazozisema hapa zimepelekwa ni fedha ambazo tunajua kwamba zipo katika utaratibu na zitakwenda. Fedha ambazo mimi zinanisumbua ni zile za maombi maalum ya shilingi 162 ambayo hayo ndiyo tutakayofuatilia pamoja na ofisi yangu pamoja na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapatikana.

Katika huu mpango mkubwa ambao tunauzungumza wa kutoka mwaka 2013 – 2015 tunaouzungumza, kiasi cha pesa kinachoombwa kama maombi maalum ambayo ipo katika *Strategic Plan* ya Wizara ya Maji, ni shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Spika, nikisema nikusomee mambo ambayo yamekusudiwa kufanywa hapa nitachukua muda mrefu sana japo nimeorodhesha, Mheshimiwa Godfrey Zambi ni rafiki yangu nita-*share* na yeye kumuonyesha kwanza kujenga mradi wa chanzo cha Mwasiana, kuzalisha mali kufikia mita za ujazo 1,296 na humo ndani tunaangalia na vyanzo vya visima na kuweka mtandao mzima wa maji na ninajua nikisoma yote hii Mheshimiwa Spika utanisimamisha. *(Makofi)*

Lakini itoshe tu kusema kwamba sisi matarajio yetu ni kwamba ikifika mwaka 2015 ahadi zote tulizozitoa katika

Ilani ya Uchaguzi zitakuwa zimetekelezwa tukishirikiana na yeye pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hofu yangu sasa ni kwamba watu wataanza kusema na ya huko inafanana na ya kwao, si kweli!

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Waziri Mkuu niongeze jibu kwenye majibu mazuri ya nyongeza yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Godfrey Zambi kwamba Wizara ya Maji imeingiza mji wa Vwawa ni kati ya miji 39 ambayo itatengewa fedha katika Bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji pale.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela!

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

Kwa kuwa, kulingana na majibu yaliyotolewa na Serikali jana Mheshimiwa Waziri wa Maji, inaonyesha kwamba Serikali ina mpango mzuri sana wa kuondoa tatizo la maji mijini mfano Dar es Salaam Jijinii.

Je, Serikali inaweza ikatuambia ina mpango gani wa uhakika wa kumaliza matatizo yaliyopo vijijini sasa kwa

sababu vijijni matatizo ni makubwa sana na ninazungumza kwa ajili ya vijiji vyote vya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kilango kwa swali zuri aliloliuza ambalo linahusu maji vijijini na ambalo linagusa Watanzania wengi.

Ni kwamba Wizara ya Maji imeanza kutekeleza mpango wa kupeleka maji vijijini toka mwaka 2007 na mpango huu ni wa miaka mitano mitano na kila wilaya ilipendekeza vijiji 10.

Sasa lipo tatizo kwamba mpango huu umechukua muda mrefu kwa sababu kwanza fedha nyingi ambazo zipo kwenye mpango huu ni fedha za nje na fedha za nje tunazopewa zinakuwa na masharti na sharti mojawapo ni taratibu za manunuzi kufuata taratibu za Benki ya Dunia, ni tofauti na taratibu zetu za ndani.

Kwa hiyo, taratibu hizi zimechukua muda mrefu lakini kufikia mwaka 2012 Juni, karibu Halmashauri nyingi zimeanza kupata vibali vya kuanza ujenzi wa miradi hii na hivi ninavyoongea Halmashauri 111 mpaka Desemba 2012 zimeshapata vibali na ujenzi sasa hivi unaendelea wa vijiji vitatu vitatu kwa kila Halmashauri.

Kwa hiyo, tunategemea kwenye mwezi wa sita, vijiji zaidi ya 300 Tanzania vitakuwa na maji ya kutosha na tutakwenda kwenye awamu ya vijiji vingine viwili vya nyongeza na baadaye vijiji vitano kati ya vile 10. Kwa hiyo, tunategemea kwamba ifikapo mwaka 2015 malengo

yaliyowekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini vilevile kwenye mpango au *vision* ya 2025 tutakuwa na 65% ya Watanzania ambao wanapata maji vijijini.

Mheshimiwa Spika ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 69

**Kuwaongezea Watumishi Ajira za Mkataba**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (K.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE)** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwaongezea Watumishi muda wa kutumikia Taifa hata baada ya kustaafu kazi, wakati taaluma zao sio adimu *(rare profession):*-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi za Serikali kufanya hivyo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuwaongezea muda Watumishi hao kunawakosesha ajira vijana na wasomi nchini?

(c) Je, kufanya hivyo siyo kwenda kinyume na misingi ya Utawala wa Sheria?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi za kutoa mikataba kwa watumishi waliostaafu ni upungufu wa wataalamu katika Sekta husika. Kifungu 12.2 cha Waraka wa Rais Na. 1 wa mwaka 1998 kinatamka wazi kwamba endapo Utaalamu wa Mtumishi unahitajika sana, Serikali inawajibika kumwomba Mtumishi kuendelea kufanya kazi na siyo Mstaafu mwenyewe kuomba.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inaendelea kuajiri kwa Mkataba Watumisni wa Kada mbalimbali na takwimu zinaonyesha kuwa kuanzia mwezi Julai, 2010 hadi Desemba, 2012 ni watumishi wastaafu 1,077 walioajiriwa kwa mkataba, wakiwemo Maprofesa na Wahadhiri wa Vyuo Elimu ya Juu, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari hususani wa masono ya Sayansi, Hisabati na Lugha, Maafisa Kilimo, Maafisa Mifugo, Mahakimu, Askari na Watumishi wa Afya.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wapo vijana na wasomi wengi waliohitimu Vyuo mbalimbali hapa nchini. Hao hupatiwa ajira kulingana na mahitaji na bajeti iliyopo. Hata hivyo, Serikali inatoa ajira za Mikataba kwa Wastaafu kutokana na kuhitajika kwao sambamba na kuajiri wahitimu wa vyuo mbalimbali. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo siyo kwenda kinyume na utawala wa Sheria bali ni kwa lengo la

kukabiliana na uhaba mkubwa wa wataalam katika Sekta husika ili kutoathiri utoaji wa huduma kwa wananchi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, katika Halmashauri zetu na sehemu nyingi nchini kuna nafasi nyingi ambazo zinakaimiwa na watu kwa hiyo unakuta Kaimu, Kaimu, Kaimu katika Halmashauri moja zaidi ya 20.

Je, sasa Serikali haioni kwamba ni afadhali kuchukua au kuwaajiri watu wengi ili kujaza nafasi hizo kwa sababu kwa sasa tuna wataalam wengi ambao hawana kazi?

Pili, kwa vile hata vijiji vyetu na Kata sehemu kubwa ni Kaimu tu, wanakaimu na kukaimu.

Je Serikali haitangazi vijiji vyote viajiri pamoja na Kata ziajiri Watendaji Kata na Vijiji ili tuwapate watu wengi ambao watapata ajira kuliko kuzagaa tu bila ajira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kama anavyosema nakubaliana naye kwamba kuna nafasi nyingi ambazo zinakaimiwa hasa kwa Wakuu wa Idara katika Halmashauri mbalimbali.

Lakini tutambue kwamba katika nafasi za Wakuu wa Idara, Mkuu wa Idara yeyote ili aweze kupata ule ukuu wa Idara badala ya kukaimu ni lazima mchakato ufanyike ili kuhakikisha kwamba huyu Mkuu wa Idara hana dosari yoyote na huo mchakato kwa kweli huwa unachukua muda mrefu.

Lakini kwa sasa hivi tumeshaainisha sehemu zote za Wakuu wa Idara ambao wanakaimu na sasa hivi tuna mpango wa kuzijaza nafasi zote za kukaimu. *(Makofi)*

Pia tutambue kwamba nafasi za kukaimu ni nafasi za watu wazoefu na siyo uajiri leo halafu umpe mtu Mkuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kuhusu nafasi za Vijiji na Kata, sasa hivi mkiangalia kwenye ratiba yetu ya shughuli za Bunge, siku ya Alhamisi na Ijumaa kuna *Miscellaneous Amendment* ambayo itakuwepo. Katika *Miscellaneous Amendment* kitu kimojawapo ambacho tutakijadili ni kutoa madaraka kwa Halmashauri na Taasisi nyingine kuajiri kada za chini. Kwa hiyo, hilo limeshafanyiwa kazi. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba ni kada ipi inayoongoza kwa kuongezewa muda baada ya kustaafu?

**SPIKA:** Umemsikia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Nimemsikia!

**SPIKA:** Haya! Majibu tafadhali!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kada ambayo inaoangoza kwa watumishi wengi ambao wanapewa mkataba ni Wahadhiri pamoja na Maprofesa wa Vyuo Vikuu, Walimu wa *Primary* na *Secondary,* Askari Polisi pamoja na Askari Magereza mwaka, 2010.

Tuliwapa mikataba kwa sababu ya shughuli za uchaguzi ambapo mikataba yao inapungua, pamoja na Madaktari na Manesi. Hizi ndiyo kada ambazo zinaongoza lakini kama anataka takwimu kamili ipo hapa nitampatia Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. APLHPAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kinachosababisha watumishi hawa waongezewe mkataba ni upungufu wa hao wataalam na kwa kuwa majibu hayo yana sura ya kuonesha kwamba Idara ya Utumishi inakuwa haijui kwamba umri wa kustaafu wa watumishi unakaribia ili waanze kujiandaa.

Je, Mheshimiwa Waziri anataka kuliaminisha Bunge hili kwamba Idara ya Utumishi haina kitu kinachoitwa *rare profession succession plan? (Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Idara ya Utumishi ina *succession plan* ambayo inafahamika katika idara zote, tulichofanya sisi Idara Kuu ya Utumishi ni kutoa mwongozo kwenye sehemu mbalimbali za waaajiri kuwa na *succession plan*. Sisi tulichotoa ni *succession plan guideline*, yaani mpango wa urithishaji wa madaraka.

Kwa hiyo, hiyo ipo na ipo katika kila Halmashauri, kila Sekta inayojitegemea ambayo ni ya Serikali pamoja na Serikali Kuu. Hizo *guide lines* ziko hapa Mheshimiwa Mbunge, kama anazihitaji nitampatia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, naomba tuendelee tumeishatoa *enough time*. Najua Mheshimiwa Ntukamazina ndiye fundi mwenyewe, naomba nimpe nafasi maana alifanya kazi kule. Mheshimiwa Ntukamazina, swali la nyongeza au huna! Okay, hana habari! (*Kicheko*)

Na. 70

**Viwanja vya Ufukweni kuuzwa kwa Wageni**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Serikali inatambua madhara ya kuuza viwanja vya ufukweni mwa Bahari kwa Wageni?

Je, Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na matatizo yanayoweza kutokea kwa maeneo haya kutumika kinyume na kuhatarisha usalama wa nchi?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua madhara ya kuuza viwanja vya ufukweni mwa Bahari kwa wageni ambayo ni pamoja na ardhi ya nchi kumilikiwa na wageni na kuhatarisha ulinzi na usalama pamoja na amani ya taifa letu, wananchi kukosa ardhi kwa ajili ya uwekezaji vitega uchumi kama vile hoteli, kuongezeka kwa uharibifu wa mazingira na kusababisha wananchi kukosa fursa ya kutumia maeneo ya fukwe za Bahari kwa burudani, michezo na mengineyo.

Kwa kutambua madhara hayo na mengine, Serikali iliamua kutunga Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Sheria ya Mipango Miji Na. 7 ya mwaka 2008 kwa lengo la kulinda ardhi na mazingira ya nchi yakiwemo maeneo ya fukwe za bahari.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 (1) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kinakataza wageni kumilikishwa ardhi yakiwemo maeneo ya fukwe za bahari isipookuwa kwamba wanaweza kupewa haki ya kutumia ardhi kwa shughuli za uwekezaji ambayo hutolewa kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya 1997.

Ili kutekeleza matakwa hayo ya sheria, Serikali ilitoa tamko kupitia Tangazo la Serikali Na. 72 la mwaka 2001 kwamba endapo kuna maridhiano ya raia kumuuzia mgeni kipande cha ardhi kwa ajili ya uwekezaji ardhi hiyo inapaswa kurejeshwa Serikalini ili Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi iyafikirie maombi ya mwekezaji mhusika juu ya ardhi hiyo na ikiridhika kuwa mpango wake unakidhi mpango ulioainishwa kwenye mpango wa matumizi ya ardhi ya eneo hilo itaidhinisha maombi hayo. Baada ya hatua hiyo mwombaji atamilikishwa kipande hicho cha ardhi kupitia Kituo cha Uwekezaji ambacho kitatoa haki ya kutumia ardhi hiyo, yaani *delivative right.*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ifuatayo kwa lengo la kulinda fukwe za Bahari:-

(i) Kuhakikisha kwamba ardhi kwa ajili ya uwekezaji inatolewa kwa idhini ya Kamati ya Taifa ya Kugawa Ardhi iliyoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 ambapo moja ya majukumu yake ni kumshauri Kamishina wa Ardhi kuhusu ugawaji wa ardhi katika maeneo ya fukwe za bahari (*beach plots*) *na* ardhi kwa ajili ya kuanzisha vituo vya huduma za kimji *(New Urban Centres).* Aidha, Kamati hiyo inahusika kumshauri

Waziri wa Ardhi kuhusu umilikishaji wa visiwa vidogo *(Small Islands).*

(ii) Kuhakiki ardhi iliyopo katika mwambao mwa fukwe za bahari kwa lengo la kujiridhisha kama umiliki na ujenzi unazingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 na sheria nyinginezo na kuchukua hatua dhidi ya wale wote waliokiuka sheria ikiwa ni pamoja na kuwashitaki mahakamani na kuondoa maendeleo yaliyofanyika katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa viko viwanja vilivyopimwa na kugawiwa waendelezaji miaka ya 1950 kabla ya sheria nilizozitaja kutungwa. Kwa kuwa wahusika walimilikishwa na mamlaka halali maendelezo yaliyopo yatabaki hadi hapo Hati zao zitakapomalizika muda au Serikali ikipata viwanja mbadala na fedha za kulipa fidia maendelezo hayo yataondolewa kabla ya muda huo kumalizika.

(iii) Kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi hususan maeneo ya fukwe za bahari ili kuhakikisha kuwa matakwa ya Sheria ya Ardhi ya 1999 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inayoelekeza kuwa upana wa mita 60 ya eneo la ufukwe linaachwa wazi kwa ajili ya matumizi ya umma. Mfano, Serikali katika kutekeleza hili iliandaa na kutekeleza Mradi wa Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari na Ukanda wa Pwani *(MACEMP).*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara yangu inaandaa Mwongozo wa Uendelezaji Visiwa Vidogo nchini kwa lengo

la kuhakikisha kuwa vinatumiwa ipasavyo kwa ajili ya uhifadhi na shughuli za utalii na maendeleo mengine muhimu bila kuathiri ulinzi na usalama wa nchi yetu. Pia Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka nyingine za Upangaji wa Mji na Usimamizi wa Mazingira inaendelea kuchukua hatua za kiutawala na kisheria kwa walioendeleza maeneo ya fukwe kinyume cha Sheria.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu marefu sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ilikataza kumilikishwa ardhi kwa wageni kwa malengo mazuri sana ya kulinda ardhi ya Watanzania na kwa kuwa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ilitoa mwanya kwa wawekezaji wa nje kumilikishwa ardhi na tumeshuhudia maeneo ambayo ni *strategic* yanamilikiwa na wageni, kitu ambacho ni hatari sana.

Je, Serikali sasa iko tayari kuleta sheria ya Ardhi Bungeni ili Bunge hili liibadili sheria hiyo wageni wawekezaji wakodishiwe Ardhi kwa kipindi cha miaka isiyozidi 20 na pale mwekezaji anapotaka Ardhi aingie ubia na Mtanzania na mchango wa Mtanzania uwe ni Ardhi yake ambayo iko ndani ya nchi yake? *(Makofi)*

Swali la pili, sasa hivi kuna ugaidi na uharamia *almost* kila mahali dunia nzima na ni vigumu kwa Serikali kujua kinachofanyika kwenye ufukwe, kwenye majumba ya kifahari na mahoteli yaliyojengwa.

Je, Serikali inafahamu kwamba majumba haya na mahoteli haya yanaweza yakatumika kama miavuli kwa ajili ya kupanga mikakati ya kufanya uharamia ndani ya nchi na hata nje ya nchi kwani yako ufukweni? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Naibu Waziri kweli majibu yalikuwa marefu mno.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa jitihada zake za kushirikiana nasi katika kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza kwamba turekebishe sheria ili wageni wawe wanakodishiwa Ardhi. Kwanza napenda kusema kwamba ukisoma vizuri Sheria ya Ardhi, ikisomwa sambamba na Sheria ya Uwekezaji, maana ya kumpa mgeni ardhi kutumia bila kumiliki ndiyo hiyo ya kumkodishia kwa sababu anatumia kwa muda fulani na baada ya hapo anairejesha.

Kwa sasa hivi mgeni anaweza akapewa kibali cha kutumia Ardhi hadi miaka 98 kwa maana ya kwamba tunapotoa ardhi kwa Kituo cha Uwekezaji wao ndiyo tunaowapa Hati, Hati ile nao wanaenda kutoa *derivative right* ambayo inakuwa na muda pungufu wa ule tuliowapa wao.

Sasa maoni yake ya kwamba tutizame sheria ili kupunguza muda huo nimeyachukua na tutayafanyia kazi ili kuona kama je, haitaathiri uwekezaji kwa maana ya kwamba kuna mwekezaji anakuja na mitambo, yaani labda anajenga kiwanda, ana shamba halafu ana kiwanda, mitambo ile *life time* yake ikawa ni miaka thelathini, ukimpa miaka 20 maana yake ni kwamba hawezi kukubali kuja kuwekeza. Kwa hiyo, tutatizama hilo kwa kuona athari zake kwa uwekezaji.

Swali la pili kuhusu matumizi ya mabaya ya majengo yanayojengwa ufukweni. Nakubaliana naye kwamba, inawezekana watu wenye nia mbaya wanaweza wakatumia vibaya majengo yale lakini napenda tu kukuhakishia kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi ndani ya nchi kavu, baharini na sisi wananchi tunapaswa kushirikiana nao kutoa taarifa pale ambapo tumeona jambo linatokea ili kuepusha Taifa letu na majanga ya hujuma. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana! Yule sijui kasimama au ameinama! Mheshimiwa Rajab nafikiri!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kuna sheria ambayo inataka mita maalum kutoka ufukweni mpaka pale ambapo majengo yanatakiwa yaanzie. Hii inakuwa takriban mita 50 mpaka 60 kutoka katika ufukwe. Tayari kuna nyumba nyingi ambazo zimejengwa chini ya urefu huo hasa mahoteli.

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuzibomoa zote pamoja na mahoteli ambayo yamejengwa chini ya mita ambazo zinatakiwa ili kulinda fukwe zetu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Wewe una mtu mwenye hoteli unataka ibomolewe au vipi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, katika majibu ya swali la msingi nilielezea kwamba wako waendelezaji wa ardhi waliogawiwa ardhi miaka ya 50. Kwa mfano eneo la *Msasani Beach,* viwanja vile vilipimwa mwaka 1953, 1954, watu wamejenga tayari hatukuwa na sheria iliyokuwa inawazuia kujenga katika ufukwe kwa wakati huo. Ndiyo tumesema kwamba nyumba zile zitaendelea kuwepo hadi Hati miliki itakapokwisha muda wake, lakini tukipata viwanja mbadala vya kuwapa watu wale na fedha za kuwalipa fidia tutawaondoa kabla ya muda huo.

Lakini pia naomba nifafanue kuhusu hoteli. Kwa kawaida tunaposema kwamba tumetoa kiwanja kwa ajili ya kujenga hoteli, tunampa mwenye hoteli kwamba ajenge hoteli majengo yatokee nyuma ya mita 60 lakini kile kiwanja kilicho mbele yake mita 60 zile anakuwa na *access* nayo kwa sababu wateja wanaokuja pale ambao ni wananchi wa kawaida na wageni wengine wana haki ya kutumia eneo lile la wazi la mita 60 lililo nyuma ya hoteli yake.

Kwa hivyo hiyo inafanyika kwa taratibu za kisheria wala hakuna ambaye atakuwa amekiuka sheria, isipokuwa

waliojenga baada ya sheria hizi kuwepo wale wote tutawabomolea.

**SPIKA:** Ahsante sana naona Mheshimiwa Eng. Mnyaa.

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru angalau kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, hawa wawekezaji wanapewa ardhi kwa mfumo wa miaka 33, 66 au 99 au 98 kama ulivyosema wewe lakini mara nyingi ni *standard* ya 99, na kwa kuwa katika umri wa miaka 99 mwekezaji anaweza akawa na vizazi yeye akawa hayuko duniani na vizazi wakaona ardhi ile ni mali yao:-

Je, Tanzania imejitayarisha vipi na mfumo huu ili kuepusha kilichotokezea baina Urusi na Alaska?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, najua una. Mheshimiwa Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, samahani!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nifafanue kwamba mtu unapokuwa na Hati miliki inapofikia ukomo iwe miaka 33, 66 au iwe miaka 99 ardhi ile inarejea kuwa mali ya Serikali, kwa hiyo, inabidi uombe ardhi hiyo upya.

Utaratibu tulionao ni kwamba kama unaona Hati yako inafikia mwisho unaleta *notes*, unaleta maombi ya *renewal* na mchakato unaendelea kama kawaida, Serikali hailazimiki kama ina matumizi mengine kukupa ardhi hiyo. Huo ndiyo utaratibu tulionao. Ahsante sana.

Na. 71

## Uwekaji wa Mipaka ya TANAPA na Wananchi wa Mbarali

**MHE. MODESTUS D. KILUFI** aliuliza:-

Mgogoro uliokuwepo kati ya wananchi wa Mbarali na *TANAPA* sasa umemalizika baada ya Kikao cha Kamati ya Maliasili na Utalii pamoja na uongozi wa *TANAPA* kwa makubaliano kwamba, katika kuweka mpaka wa *Ruaha National Park* Wilayani Mbarali itumike ramani ya awali ambayo haina mgogoro na maeneo ya wananchi.

(a) Je, lini sasa Serikali itakamilisha zoezi hilo la uwekaji mipaka il kuondoa mgogoro kati ya askari wa Hifadhi ya Taifa na Wananchi?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kutoa ushirikiano katika kumaliza shauri la mgogoro huo hasa baada ya kufikia ufumbuzi na muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mipaka iliyopendekezwa na kuridhiwa na Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya *(RCC)* itaendelea kuheshimiwa kwa kuwa inazingatia Tangazo la Serikali Na. 28 lililotolewa mwezi Machi, 2008 linalohusu upanuzi na kupandishwa hadhi Hifadhi ya eneo lililokuwa Pori la Akiba la Usangu kuwa sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kamati maalum iliundwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kushughulikia mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na baadhi ya wananchi wanaoishi kuizunguka mipaka hiyo. Kamati hiyo ilijumuisha wajumbe kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, *TANAPA,* TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, *RUBADA* na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mbarali.

Mheshimiwa Spika, Kamati hiyo ilitembelea vijiji 32 katika Wilaya ya Mbarali na Vijiji vitatu (3) katika wilaya ya Chunya vinavyopitiwa na mpaka mpya kwa lengo la kuangalia maeneo ambako mpaka umepita katika vijiji hivyo na kuongea na wanavijiji. Aidha, Kamati ilitembelea na kuongea na Taasisi mbalimbali zinazohusiana na mgogoro wa mpaka huo pamoja na Viongozi wa Serikali za Wilaya za Mbarali na Chunya na wadau mbalimbali wa Mto Ruaha na Bonde la Usangu ili kupata maoni yao kuhusu mpaka huo na mustakabali wa hali ya maji katika Mto Ruaha Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika kutekeleza majukumu waliyopewa imekutana na changamoto nyingi zilizohitaji ushirikishwaji wa wadau wengi zaidi kuliko ilivyopangwa.

Aidha, matarajio ya kumaliza kazi hiyo mapema zaidi yameingiliana na ukweli kwamba ili kupata ufumbuzi wa kudumu na wa muda mrefu utakaoridhiwa na wadau wote, Kamati imelazimika kufanya kazi kwa kina na kwa muda mrefu zaidi kinyume na matarajio. Hata hivyo, taarifa hiyo inatarajiwa kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ifikapo mwezi Juni, 2013 na Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mbarali watapata nafasi ya kufahamu maoni na mapendekezo ya kuhitimisha kazi hiyo iliyokabidhiwa kwa Kamati.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi mwenyewe pamoja na wananchi wa Mbarali hatujapokea vizuri sana majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa sababu jambo hili limechukua muda mrefu sana na wananchi wa Mbarali wanaumia na kutokuwepo mpaka unaofahamika.

Vilevile, ikumbukwe kwamba Wilaya ya Mbarali hatukuwa na Hifadhi, iliyokuwepo ilikuwa ni *Usangu Game Reserve* ambayo mipaka yake iko mbali, ilipokuwa sasa ni Hifadhi ya Taifa wananchi walihamishwa Kata nzima na vijiji vingine vingi tu na Serikali ikaandaa mpaka ambao hata sisi Wanambarali tunauheshimu. Sasa baadaye bila kuwashirikisha Wanambarali ikaja kuongezwa tu mpaka mwingine.

Sasa huu mpaka ndiyo tuliomba Serikali iangalie kwamba pale ilipokuwa imewatoa wale wananchi na kuweka mpaka ule mpaka uheshimiwe na Mheshimiwa Rais alipokuja akasema kwamba hakutakuwa na ongezeko la

mpaka la mwingine, utaheshimiwa ule ule. Sasa nashangaa hivi hii bado, bado, itakuwa bado mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, majibu haya kwa kweli hayaleti matumaini kwa wananchi wa Mbarali na kwamba vurugu na kero zinatokana na Serikali kutokutatua migogoro ya wananchi mapema. Watu wa Mbarali wanaumia, hakuna mpaka pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kauli ya Serikali inasemaje hasa baada ya Kamati ya Maliasili na Utalii kukaa na kuridhia huo mpaka uliowekwa na Serikali mapema na Mheshimiwa Rais kuja kusema mpaka utakuwa ni huo huo; sasa nini kifanyike ili Wananchi wa Mbarali wawe na matumaini na Serikali yao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAALISILI NA UTALII):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Modestus Kilufi, kama ifuatavyo:-

Uamuzi wa kuongeza maeneo ya Hifadhi ulitokea tangu mwaka 2006 na kusema kweli yalikuwa ni maamuzi ambayo yalikuwa na maslahi kwa Taifa zima; kwa sababu pale palikuwa na uharibifu wa ardhioevu na ni chanzo kikuu cha maji kwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yalikuwa ni maamuzi ambayo yalipitia kwenye ngazi zote za Serikali kupitia Baraza la Mawaziri, kupitia *RCC* ya Mbeya na yalipokwenda kwenye *RCC* ya Mbeya, kwanza,

yalitengewa mpaka, mipaka ile ikaenda kwa Wananchi, Wananchi walipoipokea ikaonekana kwamba kulikuwa na hitilafu, kuna baadhi ya vitongoji vya vijiji vilikuwa vimeingilia na vingine havigusi katika maeneo yale ya ardhioevu na nini.

Kwa hiyo, kuna mabishano mengi yamefikia hatua ambayo kuna baadhi ya vijiji kama saba ikafikia hatua vikafungua hata kesi Mahakamani Kuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, si kwamba jambo hili halijashughulikiwa; hapana, jambo hili limefanyiwa kazi. Baada ya pale, kusema kweli kama anavyosema Mheshimiwa Kilufi, Mheshimiwa Rais, akatoa maagizo mapya tena ambapo mashamba kama ya Madibira na Kapunga akayarudisha ili yapate kutumika na wakulima wakayatoa nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba, kuna kazi kubwa imefanywa, ambayo imeshirikisha wadau wote pamoja na *RCC* na Wananchi wa pale.

Mheshimiwa Spika, nilichosema ni kwamba, huu ni Mwezi Februari, tunatarajia ifikapo mwezi Juni, 2013, ambayo ni miezi minne tu kuanzia sasa, jambo hili litakuwa limefikia tamati na tunataka tufikie tamati ambayo itakuwa ridhaa ya Wananchi wote. Mheshimiwa Mbunge mwenyewe, atashirikishwa katika kufikiwa na taarifa hii ili tubadilishane mawazo na tupate ridhaa ya upande zote kwa ajili ya kuhakikisha kuwa maeneo ambayo yana uharibifu wa mazingira, yanabaki yamehifadhiwa vizuri.

**SPIKA:** Ahsante. Majibu yalikuwa marefu twende swali linalofuata, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo.

Na. 72

**Mapato Yatokanayo na Vivutio vya Utalii**

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na ina vivutio vingi vya utalii:-

(a) Je, Tanzania inaingiza mapato kiasi gani ikilinganishwa na vivutio vilivyoko nchini kuliko nchi nyingine wanachama?

(b) Je, ni wastani wa Watalii wangapi wanaoingia nchini kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAALISILI NA UTALII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Tanzania ina vivutio vingi na maarufu ikilinganishwa na Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vivutio hivyo ni pamoja na Uwindaji wa Kitalii *(Hunting Tourism*), Utalii wa Picha *(Photographic Tourism*), Utalii wa Fukwe *(Beach*

*Tourism),* Utalii wa Kupanda Milima, Utalii wa Kuangalia Ndege, Utalii wa Utamaduni (*Cultural Tourism)* na Utalii wa Mikutano. Takwimu zinaonesha kuwa, mwaka 2011 Tanzania iliingiza Dola za Kimarekani milioni 1.3 kutokana na watalii 868,000 waliotembelea nchi yetu. Aidha, mapato yatokanayo na utalii kwa Nchi ya Kenya kwa mwaka 2011 yalikuwa Dola za Kimarekani bilioni 1.5 kutokana na idadi ya Watalii milioni 1.2 waliotembelea nchi hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa wastani jumla ya watalii 771,000 huingia nchini kila mwaka. Aidha, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2011, jumla ya Watalii 3,800,000 waliingia nchini na kuiingizia nchi mapato ya jumla ya Dola za Kimarekani milioni 6.3.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa nchi jirani ya Kenya ina vivutio vichache, lakini wamejipanga vizuri kutangaza vivutio vyao kuwekeza kwenye utalii; na kwa kuwa Kenya wamejipatia mapato makubwa hata ukiangalia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri; je, Tanzania imejipanga vipi ili iweze kuwekeza fedha za kutosha kwenye utalii na kunufaika zaidi kutokana na vivutio vingi vilivyopo?

(ii) Kwa kuwa Tanzania na Kenya ni Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kwa kuwa Kaulimbiu ya Kenya inasema Njoo Kenya Uone Mlima Kilimanjaro; je, Serikali ina mpango gani kuipiku Kaulimbiu

ya Kenya ili badala ya Watalii kupitia Kenya wapite moja kwa moja Tanzania ili kuiongezea nchi yetu mapato?

**SPIKA:** Ahsante. Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba nifanye marekebisho ya majibu yangu ya awali, mapato yaliyopatikana katika miaka mitano iliyopita kwa Tanzania ni Dola za Kimarekani bilioni 6.3 siyo milioni 6.3.

Mheshimiwa Spika, Nchi jirani ya Kenya, wenzetu walikuwa wametangulia kusema hii ni biashara ya huduma; *is a service industry*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kutoa huduma hizi kuna vitu vingi ambavyo Watalii wanaangalia kama viwango, ubora wa hoteli, huduma na vitu mbalimbali. Kwa hiyo, kusema kweli kihistoria lazima tukubali kwamba, wenzetu wa Kenya katika kutoa huduma katika Sekta ya Utalii walianza kabla yetu na walikuwa wamechukua hatua za makusudi za kuboresha *Tourism Industry* yao siku nyingi.

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni, kwa sababu ya mambo mbalimbali ikiwa ni matatizo pia ya kiusalama Mombasa na kadhalika, Watalii wengi wanapendelea kuja Tanzania badala ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo na sisi hapa Tanzania viwango vyetu vya huduma za utalii vimekwenda vikiongozeka. Kwa hiyo, pamoja na hayo, tumekuwa tukijitangaza kwenye *CNN* na matangazo ya nje, Balozi zetu zimekuwa zinafanya kazi za kutosha kututangaza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndiyo maana unaona idadi yetu ya Watalii imepanda sana hadi kufikia milioni 1.3 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hii ya Njoo Kenya Uone Kilimanjaro, mimi hainisumbui kwa sababu zamani kulikuwa na ufahamu mdogo wa kijiografia, lakini siku hizi Watalii wengi wanajua kwamba, Kilimanjaro ipo Tanzania na kusema kweli tumekwenda tukiboresha huduma zinazotokana na Uwanja wa Kimataifa wa *KIA.*

Mheshimiwa Spika, Mashirika mengi ya Ndege yanatua *KIA,* kwa hiyo, tutarajie kwamba, hili suala la Watalii kuja Kenya ili kuona Mlima Kilimanjaro, litaondoka watakuja *KIA* ili kuuona Mlima Kilimanjaro.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa vivutio viliyopo nchini vingi vinapakana na Halmashauri zetu; na kwa kuwa Halmashauri hizo zimekuwa hazifaidiki moja kwa moja na uwepo wa vivutio hivyo kwa maana ya kutopata mapato ya uhakika na badala yake ni kama hisani tu. Je, Serikali inatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso, kama ifuatavyo:-

Suala la Uwekezaji, Vivutio na Halmashauri, linatawaliwa pia na *bylaws* ambazo Halmashauri wenyewe wanaweka na wanaingia makubaliano na wawekezaji wanapokwenda pale.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna vivutio pale na mtu anakwenda kuweka hoteli pale, ni matarajio yangu kwamba, ninyi wenyewe kwenye Halmashauri mtakuwa mmetengeneza mikakati ili hoteli zile au vivutio vile viwe na maslahi zaidi kwa Halmashauri zenu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani hili ni jambo la pamoja baina ya Halmashauri na Wizara ambayo inasimamia uwepo wa biashara na vivutio hivi.

**SPIKA:** Tunaenda Wizara ya Maji, Mheshimiwa Highness Kiwia, atauliza swali, kwa niaba yake Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami kama alivyosema Mheshimiwa Zambi, kabla ya kuuliza swali, niwaambiwe Wananchi wangu wa Arumeru kwamba ni kweli nimekuja huku juzi lakini nachapa kazi kweli kweli kuliko Mheshimiwa Naibu Spika.

Sasa, kwa niaba ya Mheshimiwa Highness Kiwia, Mbunge wa Ilemela, naomba swali lake Na. 73 lipatiwe majibu stahili.

Na. 73

## Hitaji la Tenki la Maji Kata ya Kirumba

**MHE. JOSHUA. S. NASSARI: (K.n.y. MHE. HIGHNESS S. KIWIA)** aliuliza:-

Kutokana na kukosewa kwa ujenzi wa tenki la maji katika maeneo ya Ibanda kumesababisha kukosekana kwa maji katika maeneo ya Kata ya Kirumba hasa maeneo ya Milimani na maeneo jirani kama Kata ya Kitangiri:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kujenga tenki jingine la maji ili kuwaondolea adha Wananchi wa maeneo hayo?

(b) Je, ni lini Mradi wa kusambaza maji ya bomba katika Kata ya Bugogwa na maeneo jirani ya Kata ya Sangabuye utakamilika hasa ikizingatiwa kuwa upembuzi yakinifu na hatua za awali za ujenzi huo vilikwishafanyika?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Wenzio hawachapi kazi! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Highness Samson Kiwia, Mbunge wa Ilemela, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, ilikamilisha ujenzi wa tenki la maji katika Kilima cha Kitangiri, lenye ujazo wa lita milioni mbili kwa lengo la kuwahudumia wakazi hao. Tenki hilo linatosheleza mahitaji ya watu wanaoishi maeneo ya Kata za Kirumba na Kitangiri. Hata hivyo, Wananchi waliojenga baadaye eneo la juu ya tenki hawapati maji kupitia tenki hilo. Katika juhudi za kusambaza maji katika maeneo ya milimani na kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mwanza, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, imetenga jumla ya *Euro* milioni 45 na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali za manunuzi ya Mtaalam Mshauri.

(b) Mheshimiwa Spika, Kata za Bugogwa na Sangabuye zinatekeleza Miradi miwili ya Maji katika Mwaka huu wa Fedha wa 2012/2013. Kata ya Bugogwa inatekeleza Mradi katika Kijiji cha Igombe kupitia fedha za maendeleo za Halmashauri kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria; na ujenzi wa mradi katika kijiji cha Kayenze utaanza mwezi huu wa Februari, 2013, baada ya Mkandarasi wa ujenzi kusaini mkataba mwezi Desemba, 2012. Mradi wa Kayenze utatekelezwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP).*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi katika vijiji vilivyobaki vya Kata za Bugogwa na Sangabuye, utafanyika katika Awamu ya Pili ya Programu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo hayaridhishi ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nimezungumza na

Mheshimiwa Highness Kiwia leo asubuhi akasema ni kweli kwamba, hili tenki lilijengwa, lakini kwa eneo ambako limejengwa linashindwa kuwahudumia watu pamoja na kwamba linajaa maji kwa sababu limejengwa eneo ambalo ni *highly elevated***.** Kwa hiyo, maji yanajaa lakini hayawafikii Wananchi na siyo Wananchi waliojenga maeneo ya milimani pekee hata wale ambao wamejenga maeneo ya chini bado maji hayawafikii. Vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema kwamba, Kata za Bugogwa na Sangabuye zinatekeleza Miradi miwili ya maji katika mwaka huu wa fedha kupitia Halmashauri. Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela anasema, Halmashauri imegawanywa na hakuna Mradi wowote ambao unatekelezwa na Manispaa ya Ilemela kwa sasa.

(i) Sasa Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela kwa niaba ya Wananchi wake angependa kujua kwanza huu Mradi ambao umetengewa Euro milioni 45 ambao unatekelezwa sasa hivi utakamilika lini ili Wananchi wa Kata hizi mbili za Kitangiri na Kirumba waweze kujipatia maji?

(ii) Hii Miradi ambayo amesema inatekelezwa na Halmashauri ambayo kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge hakuna Mradi ambao unatekelezwa sasa hivi; *timeframe* yake pia nayo ni lini?

**SPIKA:** Ahsante kwa kuwa mwaminifu kwa mwenye swali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, (a) ni kweli tenki lile lilipojengwa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Wananchi waliojenga sehemu ya juu hawapati maji.

Kilichotokea ni kwamba, usanifu wa tenki hili ulifanyika mwaka 1994 na 1995 na baada ya fedha kuonekana hazipatikani ndiyo tenki likajengwa mwaka 2007, kama nilivyosema kwa ushirikiano wa Ujerumani na Serikali yetu na wakati wakijenga lile tenki hakukuwa na watu kule mlimani. Wakati wanajenga lile tenki ililazimika kupeleka vifaa vya ujenzi na ili upeleke vifaa vya ujenzi ililazimika kuandaa barabara. Sasa baada ya kujenga tenki pale na barabara ipo pale, Wananchi wakatamani na wakaenda kujenga katika yale maeneo ambapo Halmashauri baadaye ilipima na kuruhusu Wananchi kwenda kuishi pale.

Sasa nini kinafanyika ili kuwapatia wale Wananchi maji; ipo mikakati miwili ambayo inafanywa na Mamlaka ya Maji (MWAUWASA). La kwanza, wametuma Wataalam kwenda Iringa kujifunza jinsi walivyopeleka kule milimani, kama mnavyofahamu, Iringa Wananchi wanaishi kwenye milima ya mawe kama ilivyo Mwanza, lakini wao wamefanikiwa kuweka *booster* na kupeleka maji kwenye hivyo vilima. Kwa hiyo, Wataalam kutoka MWAUWASA wameshaondoka jana na leo hii wapo Iringa wanajifunza ili watumie hiyo teknolojia kusambaza siyo kwenye hiyo sehemu ya Kitangiri na Kirumba tu na maeneo mengine ya Mji wa Mwanza. Vilevile wanaangalia *option* ya pili ya kujenga tenki dogo juu ili liweze kuhudumia wale Wananchi, ambalo litakuwa na lita kama 150 za ujazo.

Sehemu ya pili, kwamba hakuna Mradi unaotekelezwa kwenye Halmashauri ya Ilemela baada ya kugawanywa, ni kweli kuna Miradi inatekelezwa lakini inasuasua.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetembelea kwenye Halmashauri hii na nikakagua Miradi ya Vijiji Kumi. Pale kuna Mradi wa Kayenze ambao nilisomewa taarifa nilipotembelea na mpaka sasa unasuasua kwa sababu walipewa kibali mwezi Agosti na Benki ya Dunia lakini wameweza kusaini Mkataba na Mkandarasi mwezi Desemba, miezi minne baadaye. Hivi ninavyoongea, bado yule Mkandarasi hajaanza kazi na huu ni mwezi Februari. Kwa hiyo, mimi nimwombe Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela, akae na Halmashauri yake, waweze kuharakisha utekelezaji wa hii Miradi ya Vijiji Kumi kwa sababu kama hutamaliza Kayenze huwezi kuanza hiyo mingine ambayo ameitaja. *(Makofi)*

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kulikuwa na *Water Rural Supply and Sanitation Programme Phase One* na Programu hii ilikuwa ina kasoro kadhaa ikiwemo kuwa na wakandarasi wasiokuwa na viwango na maeneo mengine hata kufikia hatua ya maji kwenda kuchimbwa wakati utafiti haukufanyika na mfano mzuri ni Wilaya ya Muheza. Je, Serikali haioni kwamba ni dhihaka kwenda kuchukua hatua ya kukopa fedha nyingine kwa *African Development Bank* kwa ajili ya *Phase Two* wakati Phase ya Kwanza ilikuwa na kasoro na ripoti haijaletwa ili hatua za makusudi ziweze kuchukuliwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru kwa sababu ni mwendelezo wa msititizo kwa yale yaliyojitokeza kwenye maji vijijini na hasa kwenye

uchimbaji wa visima. Tumeeleza hapa kwamba, tatizo kubwa lililojitokeza ni kwamba, taratibu zilizotumika hazikuwahusisha Wataalam wetu wa Mabonde ya Maji ambao wana utaalam wa kuainisha ni maeneo gani yana maji. Tumesema sasa hivi tunarekebisha hilo na tumeshaanza kulifanyia kazi na yale maeneo ambayo yalishafanyiwa utafiti yakaonekana kama maji hayapo kihalali, tutafanya utafiti wa maeneo mengine ili yaweze kupatiwa maji kama sehemu zingine.

Na. 74

**Ukosefu wa Maji kwa Wananchi wa Ngudu**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Wananchi wa Ngudu, Kwimba, wanatumia maji kutoka Bwawa la Mwamasululu ambalo lina maji mazito yenye tope, tatizo linalosababishwa na uchache wa vyanzo vya maji na miundombinu chakavu ya maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru Wananchi wa Ngudu kwa ukosefu huo wa maji hali inayoweza kuleta mlipuko wa magonjwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa katika Mji wa Ngudu kuna upungufu wa maji unaosababishwa na uchakavu wa miundombinu ya uzalishaji na usambazaji wa maji. Uzalishaji wa maji kwa siku ni lita za ujazo 260,000 na mahitaji ni lita za ujazo 1,130,000. Aidha, Wananchi wa pembezoni wanapata huduma ya maji kupitia visima vinane vya pampu za mkono vilivyopo kwenye Vitongoji vya Sokoni, Nyanhiga, Ngumo na Budula.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Ngudu, Serikali katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, imetumia jumla ya shilingi milioni 71 kwa ajili ya kukarabati mitambo ya zamani na kufunga mitambo mitatu mipya katika Mji wa Ngudu. Aidha, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Ngudu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya Kwimba, imepanga kuchimba visima vitatu vya maji ambavyo vitawekewa pampu za kusukuma maji kwenye mtandao uliopo pamoja na kusafisha visima vitano vilivyopo. Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo, amekamilisha uchimbaji wa visima vitatu na anaendelea kusafisha visima vitano vilivyopo kwa gharama ya shilingi milioni 75.94. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Ngudu unakua kwa kasi, Serikali inatayarisha Mpango wa Muda Mrefu wa kuondoa tatizo la maji la Mji wa Ngudu. Hivi sasa, Serikali imeanza taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa kutumia maji ya Ziwa Victoria. Mradi huo utakuwa na chanzo cha pamoja na Mji wa Magu kwa lengo la kutumia rasilimali fedha kwa ufanisi

badala ya kujenga Mradi mingi midogo midogo kutoka Ziwa Victoria.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba tatizo la maji Ngudu linasababishwa kwa kiwango kikubwa na miundombinu iliyochakaa.

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi unaofadhiliwa na Wafaransa pamoja na *European International Bank,* ambao umeibagua Ngudu na kuhudumia Misungwi, Magu na Lamadi. Cha kushangaza, huwezi ukatoka Misungwi ukaenda Magu bila kupita Ngudu. Swali.

(i) Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kuna haja sasa ya kufanya marekebisho ya haraka ili Ngudu nayo iingizwe kwenye Mradi huu?

(ii) Suala la maji Ngudu na Kwimba kwa ujumla limekuwa tatizo sugu. Mnamo Septemba, 2012, Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua Bwawa la Mahiga baada ya kusikia kilio chetu cha Wanakwimba, lakini cha kushangaza Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua bwawa kwa ajili ya umwagiliaji wa mimea! Nimekuomba gauni unanipatia kaptura. Ninaiomba sasa Serikali iboreshe Bwawa la Mahiga na hata lile la Mwamasululu badala ya kutupatia maji kwa ajili ya mimea watupatie maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Inatosha. Haya kama kaptura siyo nguo, basi sawa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba Ngudu imebaguliwa kwenye Mradi huu mkubwa unaofadhiliwa na *European Investment Bank* na Ufaransa, siyo kweli kwa sababu nadhani hapa tungetakiwa tuishukuru Serikali kwa sababu awali Ngudu haikuwepo kwenye Mradi wa kupewa maji kutoka Ziwa Victoria. Tafiti za awali zilionesha kwamba ili tuboreshe maji Ngudu tutumie visima, lakini baadaye Serikali ikaona kwamba ile haitakuwa suluhu ya kudumu, kwa hiyo, tukalazimika kuingiza kwenye mpango wa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu ambao unafanywa kati ya Magu na Ngudu na unafadhiliwa na Programu ya *WSDP.* Kwa hiyo, sasa inapochukuliwa Magu, Misungwi na Lamadi kuingizwa kwenye hii Programu nyingine, inatoa nafasi kwa Programu ya Maji ya *WSDP* ku-*fund* huo Mradi wa Ngudu wa pekee na utawezekana. Utakapokuwa unajengwa ule Mradi wa Magu, kile chanzo ni kimoja, kwa hiyo, *automatically* Ngudu wanafaidika na kile chanzo.

Sehemu ya pili kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitembelea hilo Bwawa la Mahiga, inaonekana tunajali zaidi umwagiliaji kuliko binadamu. Mimi natambua sana kilio chako, unavyotetea Wananchi kuhusu maji, ambapo umekuwa unakuja hapa, lakini nakuhakikishia kwamba, siku Wananchi wale watakapokosa chakula, watakuja na kilio hicho hicho hapa Bungeni. Kwa hiyo, naona tuipongeze Serikali kwamba lile Bwawa kama ulivyosema mwenyewe, nakupongeza sana litatoa maji kwa ajili ya umwagiliaji, litatoa maji kwa ajili ya mifugo na litatoa maji kwa ajili ya matumizi ya Wananchi.

**SPIKA:** Ahsante. Ili nisiharibu swali lake, basi naendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Anastazia James Wambura.

Na. 75

**Tatizo la Ukosefu wa Maji Safi na Salama**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Tatizo la ukosefu wa maji safi na salama limekuwa ni kero ya Kitaifa hasa katika maeneo ya Vijiji ambako ndiyo asilimia kubwa ya Wananchi wanakoishi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kulifanya suala la maji kuwa kipaumbele cha kwanza cha Kitaifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la ukosefu wa maji safi na salama linalolikabili Taifa hasa maeneo ya Vijijini. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeandaa Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na kisha kuandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* mwaka 2006, ambayo inatekelezwa kwenye Halmashauri zote nchini. Programu hiyo inalenga kutekeleza Sera ya Maji, ambapo utekelezaji wake unafanyika kwa vipindi vya miaka mitano mitano

hadi mwaka 2025. Kwa kuanzia, kila Halmashauri iliteua vijiji kumi katika Awamu ya Kwanza ya Programu. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2012, Halmashauri 111 zimeanza ujenzi wa miundombinu ya maji na Halmashauri zilizobaki zipo katika hatua mbalimbali za kusaini mikataba ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, imeipa Sekta ya Maji umuhimu wa juu kwa kutekeleza Miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Vilevile nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

(i) Kwa kuwa hii Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inakwenda taratibu sana, kuna baadhi ya Wananchi wameamua kuchimba visima binafsi ili waweze kupata maji lakini kunakuwa na kikwazo katika upatikanaji wa vibali kutokana na ile sheria ambayo inamtaka kwamba, mtu anapotaka kuchimba kisima apate kibali kutoka kwa mamlaka za mabonde husika. Je, Serikali ina mpango gani wa kurahisisha upatikanaji wa vibali hivi ili Wananchi waweze kupata maji pasipo kuvunja sheria?

(ii) Katika maeneo mengi ya nchi yetu maji ya bomba hayanyweki bila ya kuweka *waterguard* au kuchemsha na mara nyingi kuna baadhi ya Wananchi wanalalamika kwamba wanapotumia *waterguard* wanapata matatizo ya kuhara. Kwa upande mwingine, kuna makundi kama wanafunzi, wagonjwa hospitalini,

wafanyakazi maofisini, wafanyabiashara, ni lazima wawe na angalau bajeti ya shilingi 1,000 kwa siku kwa ajili ya kununua maji ya chupa na ni jambo ambalo nadhani si wote wenye huo uwezo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba maji ya bomba yananyweka bila ulazima wa kuchemsha au kuongeza *waterguard*? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza kwa kuwapata hao wadau ambao wako tayari kuchimba visima ili kuweza kusaidiana na Serikali katika utekelezaji wa Sera yetu ya Maji ya Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba, tumeliona hilo, kwamba vipo vikwazo vya taratibu mbalimbali za kupata vibali kwa wale wanaotaka kuchimba visima. Kabla sijaja hapa Bungeni, tumeshaagiza Wizara yetu, Idara inayohusika ya Rasilimali za Maji Mijini, walete zile taratibu tuzipitie tuangalie ni vipi ambavyo vinakwamisha ili kuweza kuharakisha huo mchakato watu wapate vibali. Kupata vibali ni muhimu na taratibu lazima ziwepo ila tutazipunguza.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kuhusu hii Programu ya Maji ni kwamba, kama nilivyosema kwenye jibu letu la msingi kwamba, tumekuwa na vikwazo vya Programu hii kutekelezwa kwa sababu tumekuwa tunatumia taratibu za Benki ya Dunia. Kwa hivi sasa Halmashauri nyingi zimeshakuwa *competent* kwenye taratibu hizi na hivyo Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Miradi hii ya Maji itakwenda kwa kasi zaidi kuliko ilivyokuwa Awamu ya Kwanza.

**MHE. MANSOUR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri sana kuhusu tatizo la maji la Ngudu Mjini.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kwimba na Ngudu ni Mji wangu Mkuu, Wananchi wangu waliniomba niwasafishie Bwawa la Mwamasululu na mimi nimejipanga kulisafisha mwaka huu. Je, Serikali ipo tayari kuungana mkono na mimi ili nikipeleka mitambo yangu kusafisha Bwawa la Mwamasululu tushirikiane? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Pili, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Kwimba kwamba, Serikali itashirikiana kwa karibu na Wananchi wa Kwimba katika kusafisha Bwawa hilo.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea. Kwa sababu ya muda, Waheshimiwa tuingie Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 76

**Mnara wa Mawasiliano ya Simu wa Tigo**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA)** aliuliza:-

Mnara wa Mawasiliano ya Simu wa *TIGO* ulisimikwa miaka mitano iliyopita na kuanza kufanya kazi mapema mwezi Novemba, 2011:-

Je, ni lini Wananchi wanaoishi maeneo ya Kata za Mbaha, Ngumbo na Livundi waishio Mwambao wa Ziwa Nyasa wataunganishwa na mtandao huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Kampuni ya Simu ya *TIGO* ilisimika mnara wa mawasiliano ya simu katika Jimbo la Mbinga Magharibi. Hata hivyo, Jiografia ya maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, imesababisha maeneo hayo kutoweza kupata mawasiliano ya simu ya uhakika kutoka katika mnara huo wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCAF),* tayari imepata Kampuni itakayofikisha mawasiliano katika Kata ya Mpepai, Jimbo la Mbinga Magharibi; na kiasi cha Dola za Kimarekani 28,500 zimetengwa kwa kazi hiyo. Aidha, katika Awamu ya Pili, Serikali inakusudia kupeleka mawasiliano katika Kata za Mbaha, Ngumbo na Livundi katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

Mwisho, nitumie nafasi hii kurudia kauli ya Serikali tuliyoitoa wakati wa Kikao cha Kwanza cha Bunge hili kwamba, kufikia mwaka 2015, vijiji vyote nchini vitakuwa vimepewa mawasiliano ya uhakika.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa sawa, Kata ya Mpepai ipo katika Jimbo la Mbinga Mashariki, Jimbo langu, na pia Vijiji hivi ambavyo Mheshimiwa Kapteni Komba ameviuliza vya Mbaha, Ngumbo na Livundi haviko Mwambao wa Ziwa Tanganyika bali vipo Mwambao wa Ziwa Nyasa. Sasa maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa amesema hivi Vijiji vitapata mtandao katika Awamu ya Pili; ni lini Awamu hii itaanza?

(ii) Kwa kuwa Kata za Ukata, Vipororo na Ngima katika Jimbo la Mbinga Mashariki zipo karibu sana na Vijiji ambavyo Mheshimiwa Kapteni Komba amevitaja katika Jimbo la Mbinga Magharibi; ni lini basi Vijiji hivi au Kata hizi zitapatiwa mawasiliano ya simu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Vijiji nilivyovitaja haviko katika Mwambao wa Tanganyika bali ni Ziwa Nyasa. Nikubaliane naye.

Kuhusu lini Awamu ya Pili itaanza; Awamu ya Kwanza inapoisha, Awamu ya Pili inakuwa imeshaanza. Kwa maana hiyo, sasa hivi tayari tunaandaa tena *documents* kwa ajili ya kufanya *tendering* kwa awamu ya pili. Kwa

hiyo, tayari tumeshaanza, ni muda tu utakapokamilika basi tukishakuwa tumepata wakandarasi, tayari usimikaji wa minara utakuwa umefanywa.

Kuhusu swali la pili la vijiji jirani; ni kweli vijiji jirani anavyovisema vinaweza navyo vikapatiwa mawasiliano. Nisisitize tu kwamba, Serikali itaendelea kuweka mawasiliano katika vijiji vyote hatua kwa hatua kama ilivyoahidi na kufikia mwaka 2015 vijiji vyote vitakuwa vimefikiwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tuliona ni namna gani nchi yetu ilipata sintofahamu ya kiusalama mipakani mwa Nchi yetu ya Tanzania na Nchi ya Malawi na hivyo kusababisha kuonekana kwa umuhimu wa mawasiliano katika maeneo yote ya mipaka ya Nchi ya Tanzania ikiwemo eneo la Muhukulu mpakani mwa Tanzania na Nchi ya Msumbiji; umuhimu wa kuwa na mawasiliano kwa maana ya ulinzi wa mipaka ni kitu cha msingi sana.

Je, ni lini Serikali itatimiza azma ya kupeleka mawasiliano katika Kata ya Muhukulu mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ili kujidhihirishia usalama katika njia ya mawasiliano kama kukatokea tatizo lolote lile?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Serikali kupitia Mfuko wa *UCAF*, tumejipanga

kuhakikisha kwamba, sehemu zote ambazo wao wanaziona hazina mvuto kibiashara, zinafikishiwa mawasiliano na ndiyo sababu nikasema tayari Awamu ya Kwanza wakandarasi wameshapatikana na sasa hivi tuko katika hatua nyingine tena ya kuhakikisha *tender* zinatangazwa ili tuweze kupata wakandarasi katika maeneo hayo. Maeneo ambayo tunayapa kipaumbele ni pamoja na sehemu zote zilizoko mpakani, maeneo yaliyoko Ziwani kwenye visiwa vidogo vidogo, haya ni maeneo ambayo yamepewa kipaumbele kuhakikisha kwamba awamu inayofuatia nayo yanapatiwa mawasiliano.

**SPIKA:** Naomba niendelee kwa sababu muda wenyewe umekwisha bado tuna maswali sita. Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, uliza swali.

Na. 77

**Huduma za Kurusha Fedha kwa Mtandao**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza:-

Wananchi wengi wanafanya kazi za kutuma na kupokea fedha kupitia huduma inayotolewa na Mitandao ya Simu *(Tigo Rusha, Vodacom, M-Pesa na Airtel Money)*:-

(a) Je, Usalama wa huduma hizo ukoje?

(b) Je, Serikali inafaidika vipi na huduma hii kwani fedha zinatembea ovyo katika mitandao?

(c) Katika kipindi cha 2010 - 2012 Serikali imepata mapato kiasi gani yanayotokana na biashara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, usalama sa huduma za kutuma fedha kutumia mitandao au simu za mkononi huanzia katika leseni anayopewa mtoa huduma ambazo hutolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA).* Vilevile kabla ya kuanza kutuma pesa, Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)* hutoa leseni kwa ajili ya huduma za kifedha. Aidha, katika kuhakikisha usalama wa fedha za Wananchi, mtoa huduma hutakiwa kutoa kiasi cha fedha kama dhamana ambayo husimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania *(BoT)*, kwa ajili ya kulinda fedha za watumiaji wa huduma hiyo. Mwananchi kwa upande wake, anawajibika kuhakikisha usalama wa huduma za fedha kupitia simu za mkononi kwa kuzingatia masharti ya usalama kutuma na kupokea fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ujumla inanufaika na huduma hii kutokana na kuongezeka kwa miamala inayotokana na huduma hii ambapo Makampuni husika yanatakiwa kuwasilisha Serikalini kodi kulingana na miamala iliyopatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, huduma zitolewazo kupitia mawasiliano ya simu za mkononi ni pamoja na *Voice*, *SMS, Data* na *Mobile Banking.* Mapato yatokanayo na huduma hizi huchanganywa pamoja na hulipwa kwa pamoja *TRA* kama kodi ya mapato na Kampuni husika kutokana na faida ya Kampuni. Hata hivyo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa kuweka utaratibu utakaowezesha Makampuni hayo kuweza kuona mapato yanayotokana na kila huduma hususan kuanzisha utaratibu au mfumo *(Telecom Traffic Monitoring System),* utakaowezesha kujua kwa uhakika kiwango halisi cha mapato yatokanayo na huduma ya *Mobile Banking* na pia mapato yatokanayo na huduma zingine za *Voice, SMS* na *Data,* hatimaye kuimarisha udhibiti na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**MHE. MARIAM N. KISANGI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali la nyongeza, kwa kuwa ninawasemea wajasiriamali, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wajasiriamali wangu wote wa Mwenge waliopatwa na ajali ya moto.

Mheshimiwa Spika, sasa swali, kwa kuwa biashara ya kurusha pesa ya *Tigo, Voda* au *Airtel*, imetoa ajira kubwa kwa vijana Tanzania nzima na kwa kuwa faida wanayoipata wajasiriamali hao, ni asilimia mbili kwa masharti kwamba wauze na bidhaa nyingine kama *DSTV*, Luku na *DAWASCO*, ina maana faida hiyo inatolewa kwa masharti na hiyo asilimia mbili ni ndogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasimamia wajasiriamali hawa

wadogowadogo ambao wamejiajiri wenyewe nao waweze kupata faida ya kuridhisha?

Swali la pili, kwa kuwa kumezuka wizi wa fedha kupitia mitandao ya simu za mikononi na mimi mwenyewe ni mmojawapo ambaye nimeibiwa kwa njia hiyo. Je, Serikali imejipanga vipi katika kulitatua tatizo hili kwa haraka ambalo lipo katika mabenki ya NMB na Benki nyingine nyingi sana? Pesa zinaibiwa, unakuta unaambiwa kwenye mtandao akaunti yako inatoa pesa wakati humjui nani anayetoa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru kwa kutambua kwamba makampuni haya ya simu kwa kutumia huduma ya kusafirisha pesa, yametoa ajira kwa vijana na wanajipatia kipato kama njia halali ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu asilimia mbili, tuangalie hili kama suala la biashara. Sasa kama ni biashara, vijana wanapata pesa kiasi fulani lakini tukisema wapate faida kubwa sana inawezekana tena gharama ya utumaji ikawa kubwa zaidi nalo likawa ni tatizo. Kwa hiyo, hili ni suala la kuliangalia kibiashara na cha muhimu zaidi Serikali imejipanga vizuri kwa kutumia *TCRA* na Benki Kuu kuhakikisha kwamba biashara hizi zinafanyika kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuzuka kwa wizi katika mabenki, labda niwaombe Watanzania wenzangu, mara

nyingi hizi huduma zina pande mbili. Kuna uwajibikaji wa Benki ambayo yanawajibika kutunza siri na kutunza zile pesa za mteja na sisi kama watumia huduma, tuna wajibu wa kutunza zile namba zetu za siri. Mara nyingi imetokea mtu unapigiwa simu unaongea na mtu halafu una-*disclose* hiyo namba yako ya siri. Sasa kama mtu ukishampa namba yako ya siri ni sawasawa na mtu kumpa ufunguo wa kwenye *safe* yako. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba namba zetu za siri tuhakikishe hatumpi mtu yeyote hata kama ni mtoto.

Na. 78

**Kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Ushirika**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Ibara ya 76(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 inaelekeza Serikali kuhamasisha uanzishwaji wa ushirika na kuitaka iandae wataalam wengi wa Ushirika ambao wataajiriwa na kuboresha Sekta ya Ushirika nchini kote:-

(a) Je, Serikali imejiandaaje kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuipatia watumishi wa kutosha ili kuweza kusimamia uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika nchini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifufua Kada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na kuwafanya Wakaguzi hao kuwajibika moja kwa moja kwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Serikali imeandaa Muswada ambao umeshasomwa hapa kwa Mara ya Kwanza Bungeni unaokusudia kutunga Sheria Mpya ya Vyama vya Ushirika. Sheria hii itaanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo ni chombo cha kujitegemea. Muswada unaopendekezwa unaainisha utekelezaji wa majukumu ya Tume hususan ya uhamasishaji maendeleo ya Ushirika *(promotional functions)* na ya usimamizi na udhibiti *(regulatory functions).*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mapendekezo hayo, Mtendaji Mkuu wa Tume atakuwa Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na atakuwa huru kutekeleza majukumu yake. Mara Sheria hii itakapopitishwa na Bunge lako Tukufu, Tume itatenga fedha za kutosha katika utekelezaji wa majukumu hayo ya ushirika ambayo ni pamoja na yale yanayopitia mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuajiri Maafisa Ushirika wa kutosha watakaosimamia uanzishwaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya asiyeongea anyamaze ipo. Sasa imekuwa kama ni genge la kuzungumza humu ndani.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika...

(b) Serikali kupitia Tume hiyo imejipanga kufufua Kada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika hususan katika utekelezaji wa jukumu la usimamizi na udhibiti. Sheria mpya imezingatia kuwa majukumu ya usimamizi na udhibiti yanaanzia ngazi ya Serikali za Mitaa hadi ngazi ya Serikali kuu kwa watumishi wa Kada ya Ukaguzi *(Cooperative Inspectors)* ambao watawajibika moja kwa moja kwa Marajisi wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria mpya inakusudia kuainisha kwa kina suala muhimu la wajibu na dhamana ya kila mmoja wetu hususan watumishi, waajiriwa wa sekta ya ushirika, lakini kwa namna ya kipekee wajibu, dhamana na majukumu ya viongozi ndani ya ushirika wenyewe. Hii ni pamoja na hatua za kuongeza uwezo wa watumishi wa kada mbalimbali unatarajiwa kuboresha maendeleo ya ushirika nchini.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa jukumu la msingi la Idara ya Maendeleo ya Ushirika ni kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika pamoja na kuvisimamia lakini kwa utaratibu tulionao sasa, jukumu hili kwa kiwango kikubwa linatekelezwa na Serikali za Mitaa kwa kutumia Maafisa Ushirika wachache sana wanaoajiriwa na Halmashauri za Wilaya pamoja na

Sekretarieti za Mikoa. Sasa nataka nijue Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya ushirika, inahakikishaje kwamba jukumu lake hili la msingi linatekelezwa ipasavyo?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inajipanga kufufua kada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ambayo kimsingi ni Kada ya Ukaguzi wa Mahesabu na kwa vile kada hii ilishazorota kwa muda mrefu sana, je, Serikali iko tayari kuandaa programu maalum ya kuwapa mafunzo Maafisa Ushirika watakaoteuliwa kama *Cooperative Inspectors*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chibulunje ni miongoni mwa Waandamizi Wakuu katika sekta hii nchini, kwa hiyo anayoyasema anayafahamu vizuri na mimi mwenyewe huwa nakwenda kwake kupata ushauri wa maeneo haya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema kwamba katika suala la ushirika, kuna masuala ya kuhamasisha, kusimamia na kadhalika ambayo yanakwama katika ngazi ya Halmashauri. Ndiyo maana kwenye jibu langu nimesema kwamba, kwanza kabisa kwenye ngazi ya Halmashauri yenyewe tunaweka uzito kwenye suala la ushirika kwa sababu bila kuhimiza suala la ushirika hatutasogea mbele katika uzalishaji wa kilimo lakini ushirika utakwenda pia kwenye maeneo ya *agro-processing.* Ndiyo maana nasema Sheria mpya itaingiza suala la wajibu na dhamana yetu sisi wote katika kuhakikisha kwamba katika ngazi zote za Serikali kwa maana ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu,

Wizarani tunakuwa tunawajibika zaidi katika kuhakikisha kwamba yule mtendaji kule chini anafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili swali la ukaguzi, ni kweli, kimsingi ni suala la ukaguzi wa mahesabu na mwaka huu hata kwenye Vyama vya Ushirika wa Korosho tumeshuhudia kwamba vyama vingi vya Mkoa wa Mtwara na Pwani wamepata matatizo makubwa katika ukaguzi wa mahesabu yao.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa, ni kweli tutafanya mafunzo ya ukaguzi lakini jambo lingine ambalo tunatarajia litatusaidia ni kuwa na *off-sites supervision* kwa maana ya kwamba tutaweka mitambo kupitia mambo ya TEHAMA na digitali ambayo itawezesha mtu akiwa Dar es Salaam lakini anaweza kudhibiti hesabu zake akiwa Newala au akiwa Tunduru au akiwa popote alipo.

Na. 79

## Ugonjwa wa Mnyauko wa Migomba

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa zaidi ya miaka mitano sasa, Mkoa wa Kagera umevamiwa na ugonjwa wa mnyauko wa mimea hasa migomba na jitihada za kupambana na ugonjwa huo ambao uliingia nchini kutoka Uganda bado hazijafanikiwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali isitumie njia za kisayansi kwa kuharibu mimea iliyodhurika kwa eneo lote lililodhurika?

(b) Je, Serikali ipo tayari kufanya tathmini na kupunguza makali ya njaa inayotokana na kuathirika kwa migomba kiasi cha kutokutoa mazao hasa katika Wilaya ya Muleba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa mnyauko wa migomba hujulikana kama mnyauko wa bacteria. Kwa kitaalam huitwa *banana bacterial wilt* na husababishwa na vimelea vya bacteria wanaoitwa *(Bacterium Xanthomona campestris pv. Musacearum)* ambao hushambulia aina zote za migomba. Athari zake ni pamoja na kunyauka na kukauka kwa au dume, majani, kukauka kama yaliyopitishwa kwenye moto na wakati mwingine hubadilika rangi na kuwa njano. Ndizi changa kuiva kabla ya kukomaa, ndizi kuiva bila mpangilio kwenye mkungu na kuwa ngumu na endapo zikimenywa kutoa harufu mbaya na shina la mmea ulioathirika linapokatwa hutoa utomvu wa njano. Ugonjwa huu uliingia nchini kutokea Uganda na kwa mara ya kwanza ulionekana katika kijiji cha Kabare, Tarafa ya Izigo, Wilayani Muleba mwezi Septemba 2005. Kwa hivi sasa umesambaa katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera. Mbali na Mkoa wa Kagera, ugonjwa huu umeonekana Wilaya za Tarime na Wilaya ya Ukerewe pamoja na Kibondo Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia watafiti wa kilimo, Kituo cha Utafiti Maruku na asasi nyingine za kitaifa na kimataifa, wamependekeza njia za kuangamiza mimea kwenye shamba lililoathirika sana zaidi ya asilimia 75. Njia hizo ni kung'oa mashina yote na kuyakatakata ili yaweze kukauka, kutumia dawa ya kuua magugu mapana iitwayo 2-4D. Aidha, dawa hii inashauriwa kutumika tu kwenye shamba ambalo limeathirika kwa kiwango kikubwa. Kwa shamba ambalo halijaathirika sana, inashauriwa kung'oa mashina yaliyoathirika tu kwani yale ambayo hayajaathirika yataendelea kumpatia mkulima chakula.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba chakula kikuu cha wakazi wa Muleba ni ndizi, pia wanalima mazao mengine ya chakula kama vile mahindi, viazi na mihogo. Tathmini iliyofanywa na Wizara yangu kwa mwezi Januari 2013, kwa maana ya mwezi uliopita, imebaini kuwepo kwa idadi ya wananchi 8,900 katika vijiji 15 vya kata za Nyakatanga, Rutolo, Muhutwe, Mayondwi, Kagoma, Kasarunga na Burangula wanaohitaji tani 300 za chakula cha msaada ili kusaidia kupunguza makali ya njaa katika Wilaya hiyo. Taarifa hii inafanyiwa kazi na Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa lengo la kutoa chakula hicho kwa kaya zilizoathirika.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, naomba nitumie dakika moja kumweleza Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali kama ingesoma kumbukumbu za Bunge za tarehe 20, 21 na 23 Julai, 2012 isingenipa majibu

haya. Majibu haya si sahihi. Naomba nimwulize swali kutokana na majibu yake.

Mheshimiwa Spika, nilipendekeza katika swali langu la msingi kwamba mbinu za kisayansi zitumike. Utafiti wa wataalam unaonyesha kwamba Mkoa wa Kagera, ufahamu wa ugonjwa ni asilimia 93, Uganda ni asilimia 74 na Rwanda ni asilimia 61. Udhibiti wa magonjwa kwa Kagera ni asilimia 13, kwa Uganda ni asilimia 55 ambako kunasifika na kwa Rwanda ni asilimia 47. Ninachomwambia Mheshimiwa Waziri ni kwamba kunakosekana mbinu za kisayansi.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake anasema wanapendekeza, mimi sisemi kupendekeza, swali ni kutumia mbinu za kisayansi ambako *government* ina-*take lead role* ambapo kwenye suala ambalo nimezungumza kwenye nukuu ya *Hansard,* nimesema katika pesa mlizo- *ring fence* kwa ajili ya maambukizi, kitengwe kiasi kikubwa cha pesa twende kumaliza ule ugonjwa kwa kutumia mbinu za kisayansi. Ninatumia kumbukumbu kwenye *ipod* za Serikali. *This is information from the government itself.* Kwa nini msitumie njia za kisayansi ambazo mimi nimependekeza na Waziri nimekupa barua na tumekaa wote na Mkurugenzi wa *Plant Protection,* nimemwelekeza na amenielewa, kwa nini mnaitelekeza Kagera tupoteze chakula? Swali la kwanza.

Swali la pili, katika tathmini ambayo sikubaliani nayo Mheshimiwa Waziri, Kata ya Rutolo itapewa chakula kwa sababu ya kudhurika kutokana na ugonjwa wa mnyauko. Si kweli, tuweke kumbukumbu sawa na Mheshimiwa Waziri

Mkuu anasikia. Rutolo inapata matatizo kwa sababu maswahiba wa Serikali wanachunga ng'ombe wao kwenye mashamba ya wananchi, wanabaka watu, wanalisha kwenye migomba, wanachoma nyumba na nyumba zaidi ya 40 zimechomwa, kwa hiyo, mazao yanaharibiwa ndiyo maana wanakosa chakula.

Mheshimiwa Spika, sasa niulize swali; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembea katika Jimbo langu, tukaenda Buganguzi, akawaahidi wananchi kwamba matatizo ya mnyauko atayasimamia na mimi nimefanya *research* yangu na nimeshakuja na mbinu za kisayansi, ni lini atawaondolea adha wananchi wa Rutolo, ni lini ataondoa ugonjwa huu kwa kuchukua pesa *ring fenced* kwa ajili ya kutatua tatizo *once and for all? (Makofi)*

**SPIKA:** Swali lenyewe ni moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi, mbinu za kisayansi, ndiyo hilo tu basi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yenye hisia kali ya Mheshimiwa Mwijage, ni kweli alizungumzia suala hili tarehe 20 Julai lakini baada ya hapo tumetoka mimi na yeye tumekwenda ofisini kwangu na nimemwitia wataalam wa masuala haya. Yeye ni mtaalam wa mafuta, mimi ni mtaalam wa fedha na uchumi. Tumekaa na wataalam wenye jambo lao na ni kweli alikuwa ameshalifanyia utafiti wa kina na akaongea nao na akawaambia kwamba wenzetu kule Uganda wametengeneza utaratibu ambao unawawezesha wao kudhibiti ugonjwa huu kwa namna

ambayo ina ufanisi zaidi kuliko tunavyofanya sisi huku Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa aliweka ombi kwamba Idara ya *Plant Protection* ambayo ndiyo inashughulikia kinga ya mimea, ndiyo kazi yake, ifanyie kazi suala hili kwa kuzingatia pia ushauri wa kitaalam alioutoa na ushauri huo alioutoa hauendi kinyume na huu ushauri wa kitaalam ambao nimeusema hapa kwamba ndiyo njia ya kudhibiti mimea hiyo. Lakini kama anavyosema, mwanzoni kulikuwa hakuna ufahamu wa namna ya kudhibiti ugonjwa wa mnyauko kwa Mkoa wa Kagera kwa kiasi hicho, sasa hivi zaidi ya asilimia 85 wanafahamu namna ya kudhibiti unyauko, ni kweli.

Mheshimiwa Spika, naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kufanya kazi pamoja na kwamba Wizara yangu itatenga pesa kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu na hakuna haja, ulipendekeza watu waende Uganda kutazama wanavyofanya wenzetu, hakuna haja. Tunafahamu namna ya kudhibiti ugonjwa huu lakini ni lazima Serikali ya Mkoa, Wilaya na Mheshimiwa Mbunge sisi wote tuwasihi wananchi, ukiona ugonjwa kata mmea, usiubembeleze vinginevyo bacteria yule anasambaa kwa mimea mingine.

Mheshimiwa Spika, hii ya Kata ya Rutolo na kwamba kuna maswahiba wa Serikali ambapo nyumba zaidi ya 40 zimechomwa, wafugaji ndiyo wameharibu mimea, hili nadhani ni la Waziri wa Mambo ya Ndani. Lakini mimi nasema kwa sababu kuna tatizo la njaa na tathmini

imeshafanywa kwamba kuna mahitaji ya tani 300 kwa maeneo yote hayo, sisi tunalifanyia kazi ili tupeleke mahindi tuliyokuwanayo ili yakadhibiti hali ya njaa ambao huo ndiyo wajibu wangu.

**SPIKA:** Naomba niendelee na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Christowaja Mtinda atauliza swali hilo.

Na. 80

**Biashara ya Kuuza Binadamu Nchi za Nje**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Hivi karibuni vyombo vya habari vilitangaza kuwa hapa nchini kumekuwa na matukio ya biashara haramu ya kuuza binadamu hususan vijana nchi jirani kama Ethiopia kwa ajili ya kuchimba madini:-

Je, Serikali inawaeleza nini Watanzania kuhusu biashara hiyo kwa kuwa inasemekana vijana hao hupata mateso makubwa na njaa kali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hapa nchini na dunia nzima kumekuwa na matukio ya biashara haramu ya binadamu. Tanzania imekuwa ikichukua hatua mablimbali

kwa ajili ya kukabiliana na biashara hii. Hatua mojawapo ni kutunga Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu yaani *Anti-Human Trafficking Act No.6 of 2009,* na kuanzishwa Kitengo Maalumu ndani ya Jeshi la Polisi cha kupambana na uhalifu huu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matukio ya biashara hii, ni pamoja na tukio la vijana wawili wa Kitanzania waliosafirishwa kwenda Ethiopia kwa kudanganywa kuwa watapatiwa ajira nzuri kwenda kwenye Migodi ya Madini na badala yake vijana hawa wakaishia kufanyishwa kazi bila malipo na kupata mateso mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Taasisi ya Polisi wa Kimataifa yaani *Interpol,* nchi yetu inaendelea kuwasiliana na nchi mbalimbali ili kubaini mtandao wa biashara haramu ya binadamu na kuitokomeza, sambamba na kuwabaini wahanga wa biashara hiyo ili kuwarudisha nchini mwao.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ilielezwa kwamba biashara hii haramu inafanywa na wafanyabiashara wa Kenya wakishirikiana na wafanyabiashara wa Kitanzania na tangu tatizo hili lilipotokea Juni mwaka jana ni takribani miezi sita sasa hatujasikia Serikali ikisema chochote. Je, mpaka muda huu, Serikali imeshawakamata wafanyabiashara hao haramu ambao walitajwa katika vyombo vya habari? Je, Serikali kwa kuzingatia kuwa tuna mashirikiano ya Kibalozi katika nchi zetu tatu haioni kuwa tulitakiwa pia Watanzania tuelezwe jinsi ambavyo wafanyabiashara hawa wanafanya biashara hiyo ili tuwatambue?

La pili, kwa kuwa Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu ipo na tulitegemea kuwa ingefanya kazi yake sawasawa, Serikali imepata fundisho gani kutoka kwa vijana wake na watoto wadogo wa miaka 10-14 kuendelea kutoroka na wengine kutoroshwa kama ambayo tulisikia wiki mbili zilizopita ilhali nchi yetu ina rasilimali nyingi za kutosha yakiwepo madini?

**NAIBU WA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu tukio ambalo liliripotiwa kwenye vyombo vya habari la Watanzania wawili kupelekwa Ethiopia, ninaomba nitoe taarifa kuwa wahusika wawili walikamatwa nchini Arusha na wakapelekwa Mahakamani na hatia ikawapata wakatakiwa wafungwe vifungo vya miaka mitatu au kulipa faini ya shilingi milioni 10.6 kila mmoja. Watanzania hawa waliohusika majina yao yako wazi na mtu ambaye anayehitaji anaweza kuyapata kupitia Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendelea kwa tatizo hili kwa kuanzia, linahusu familia na jamii kwa ujumla na kinachoendelea sasa hivi kikubwa ni kutoa elimu kwa jamii na familia kuhakikisha kuwa kila mmoja wetu anadhibiti kutokulifanya suala hili, kwa sababu biashara hii haiwezi kufanyika kama Watanzania hatukuhusika. Kwa hiyo, elimu itaendelea na ninafikiri ndiyo msingi wa kuhakikisha mambo haya tunayakamilisha. Pamoja na hivyo, jambo linaloendelea ni kuwasiliana na Taasisi za Kimataifa, nchi jirani pamoja na *Interpol* ili kuhakikisha kuwa siyo tu kuwapa uzoefu na elimu watu wetu lakini pia kushirikiana katika mitandao ambayo mara nyingi ni ya Kimataifa kuliko Taifa.

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata na muda umepita sana ndugu zangu.

Na. 81

**Kufikisha Umeme – Tandahimba**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya umeme kati ya Mtwara – Tandahimba hadi Newala:-

Je, ni lini Serikali itafikisha umeme kwenye vijiji na Kata zote zilizopitiwa na *line* ya umeme Wilayani Tandahimba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme Wilayani Tandahimba ikiwemo miradi ya kufikisha umeme katika Vijiji na Kata zote zilizopitiwa na njia ya umeme kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatekeleza mradi wa kupeleka umeme

katika kijiji cha Mbambakofi ambapo ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita moja (1) na ufungaji wa transfoma unaendelea. Mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kupeleka umeme kwenye Kata na vijiji Wilayani Tandahimba kwa mchanganuo ufuatao:-

(a) Kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji vya Namikupa, Madaba na Kitama itajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33, urefu wa kilomita 15, njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 15 na ufungaji wa transfoma sita (6); nne (4) za kVA50 na mbili (2) za kVA 100 ili kuwaunganisha wateja 210. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania milioni tisa sitini na tatu mia sita hamsini elfu tu (963,650,000).

Aidha, zabuni za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza kazi hizi imetangazwa Desemba, 2012 kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* na ujenzi wa miundombinu ya mradi huu unaotarajiwa kukamilika ndani ya miezi 24 unatarajiwa kuanza katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2012/2013.

(b) Kazi ya kupeleka umeme kwenye Kata na Vijiji vya Mbambakofi, Nanyamba, Malamba, Miule, Diduma, maeneo ya Mji Mpya, Mnyemilo, Nanyanga, Masaki, Malopelo na Shell, inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovuti 0.4, urefu wa kilomita 15.75 na ufungaji wa transfoma sita (6); tatu(3) za kVA 50 na tatu (3) za kVA 100 ili kuwaunganisha wateja 374. Gharama za mradi

zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania milioni mia sita hamsini na mbili mia nne elfu tu (652,400,000).

Mheshimiwa Spika, miradi ya vijiji vilivyoorodheshwa hapo juu (b) imekwishanza kutekelezwa kuanzia mwezi Agosti, 2012 na inaratarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2013. Miradi ya Nanyamba, Malamba, Miule, Diduma, maeneo ya Mji Mpya, Mnyemilo, Nanyanga, Masaki, Malopokelo na Shell imekamilika kwa wastani wa asilimia 23.4 wakati ule wa Mbambakofi umekamilika kwa asilimia 100.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba kumpongeza Naibu Waziri kwa jambo moja kwamba kwenye mchakato wa hii miradi iliyokuwapo, vijiji hivi vya Namikupa ambako ni Makao Makuu ya Tarafa, Kitama na Madaba haikuwapo kwenye mpango, lakini mimi kama Mbunge wa Jimbo hilo nilipowatembelea ofisini kwao walinisikiliza na kwa hiyo, kuniweka kwenye mpango, kweli ni wasikivu, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nina maswali mawili madogo. La kwanza, Wilaya yetu ya Tandahimba na Halmashauri yetu nzima tumeweka utaratibu na tulishirikiana na *TANESCO* kuweka bajeti ya kuunganisha umeme kwenye Tarafa zetu tatu za Namikupa, Littehu na Mahuda na kwamba Naibu Waziri alipotutembelea aliona mpango huu kuwa ni wa msingi na wa kujenga maendeleo ya wananchi wa Tandahimba na kwamba aliukubali na kuahidi kuwa angeupeleka *REA* kwa ajili ya kuanza mchakato wa *implementation* lakini ninapopewa majibu haya sioni jambo hili, ningependa kupata majibu ya Serikali wanaanza lini mpango huu?

La pili, pale tunayo Tarafa kongwe ya Mahuta ambayo wananchi wamekuwa wakipata umeme pale lakini wanatumia gharama kubwa kwenda Newala kulipia ankara zao jambo ambalo linatumia shilingi 10,000/= kwenda kulipa bill ya shilingi 2,000/=. Hivi kwa nini wasiweke kituo pale au twende na wakati sasa tuwawekee Luku wananchi wale ili waondokane na adha ya kusafiri mbali pasipo sababu za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa pongezi, kwa niaba ya Wizara lakini pia nikiri kuwa ni kweli Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Simbachawene alitembelea eneo hili na kupokea bajeti kwa mkono wake mwenyewe ya vijiji na Tarafa ambazo zilikuwa bado hazijapatiwa umeme, ambazo zimepitiwa na nguzo kubwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ile tumeipokea tayari tukiwa tumeshatengeneza bajeti ambayo inatekelezwa sasa hivi na nipende kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa bajeti ile tunaiingiza katika mipango ya matayarisho ya bajeti yetu ya 2013, ambayo tunaendelea kuiandaa sasa hivi na ninamhakikishia kuwa miradi hiyo yote tutaitekeleza kama ambavyo tunaendelea na miradi mingine katika maeneo mengine ya nchi ambako *REA* imeendelea kutekeleza miradi mingi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hili suala la ofisi, ninaomba tulichukue na tulifanyie kazi na *TANESCO* kuona uwezekano

wa kufungua kituo kidogo pale cha kutoa huduma katika maeneo haya ambayo tunayaunganishia na umeme.

Na. 82

## Miradi ya Umeme ya *MCC*- Jimbo la Lushoto

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Miradi ya umeme inayofadhiliwa na *MCC* hususani Wilayani Lushoto kwa kipindi kirefu haionyeshi dalili ya kutekelezwa:-

(a)Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya utekelezaji wa miradi hiyo katika Jimbo la Lushoto na Wilaya kwa ujumla?

(b)Je, miradi hiyo itatekelezwa katika maeneo gani na kwa gharama gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.STEPHEN J. MASELE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi ya *MCC* itatekelezwa kama ilivyopangwa na mkandarasi *Symbion Power LLC* kutoka Marekani na amekwishaanza utekelezaji wa miradi hii katika Mkoa wa Tanga ikiwa ni pamoja na Jimbo la Lushoto na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ina jumla ya maeneo yapatayo kumi ambapo miradi hii inatekelezwa. Maeneo hayo ni pamoja na Yoghoi, Kwapada, Lushoto *State Lodge,* Sinza & Shimoni, Chuo cha Mahakama, Kongei , Mkuzi, Kwefingo, Irente Chini na Irente Juu. Kazi ya kupeleka umeme katika maeneo yaliyotajwa hapo juu inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilomita 8.19, njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 44.86 na ufungaji wa transfoma tisa (9). Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi za Kitanzania bilioni moja milioni mia sita themanini na mbili elfu mia nne sabini na moja elfu tu (1,682,471,000).

Mheshimiwa Spika, mradi huu umeshaanza na hadi kipindi cha taarifa hii, njia ya msongo wa umeme wa kilovoti 0.4 imekamilika kwa asilimia 100 maeneo ya Yoghoi, Kwapada, Lushoto *State Lodge* na Kongei. Kwa Irente Chini kazi imekamilika kwa asilimia 43.6 wakati wa maeneo ya Sinza na Shimoni nguzo za njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 zimesimama zote. Kwa upande wa Kijiji cha Irente Juu mashimo yamechimbwa tayari kwa kusimamisha nguzo. Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 pamoja na ufungaji wa transfoma bado haujaanza. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2012/2013.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubali kumpongeza Waziri kwa jibu zuri lakini pia niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wa miradi ya umeme kwa sasa, nilipouliza swali hili nilikuwa nina wasiwasi kuwa miradi ya *MCC* kipindi cha

utekelezaji kingeishia mwaka 2012 na kwa bahati nzuri Waziri ametuthibitishia kuwa miradi hii itaendelea.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa miradi hii katika eneo la Jimbo la Lushoto imetekelezwa kwa asilimia siyo zaidi ya 50% na kwa kuwa, muda wa utekelezaji wa mradi ulikuwa uishie Desemba 2012, je, Serikali inatuhakikishia kwamba maeneo yale ambayo mradi haujaanza kama vile Kwefingo na Mkuzi, ratiba ya utekelezaji itakuwepo?

La pili, kutokana na kucheleweshwa utekelezaji wa mradi huu, kuna maeneo ambayo mradi huu umeingiliana na utekelezaji wa *TANESCO*, kwa hiyo, utakuta kuna maeneo kuna nguzo ya *MCC* na nguzo ya *TANESCO* yenyewe. Kutokana na uwiano huu usioeleweka, Serikali inalijua hili ili tusipoteze rasilimali za nchi kwa kuweka nguzo nyingi katika eneo dogo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara, ninapokea pongezi hizi na nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba miradi ya *MCC* yote itaendelea kutekelezwa na Tanzania ni moja kati ya nchi mbili Afrika zilizofanikiwa kufaulu kupata tena mradi wa *MCC II.* Kwa hiyo, miradi yote ambayo ilikuwa imepangwa kwenye *MCC*, ninataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa itaendelea kutekelezwa kwa kuwa tutakuwa tunatenga fedha kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusu maeneo ya Lushoto ambayo kuna mradi wa *MCC* unaotekelezwa na wakati huohuo *TANESCO* nayo ina miradi yake mingine inatekelezwa, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwaagiza *TANESCO*, miradi yote hii iwe ya *REA*, *MCC,* yote hii mwisho wa siku itasimamiwa na *TANESCO*. Kwa hiyo, *TANESCO* ni lazima wasimamie kuhakikisha zile ramani wanazotayarisha kwa ajili ya miradi mbalimbali zinaenda sambamba na mipango yao wao wenyewe na siyo kuacha kwamba huu ni mradi wa *REA, TANESCO* wasisimamie na unakuta sehemu zingine miradi hii inalipuliwa. Nimetembelea Namanyere, kulikuwa na ulipuaji wa mradi wa *REA* lakini viongozi wa *TANESCO* wanasema huu ni mradi wa *REA*. Miradi hii yote ni ya Serikali na ni miradi ya wananchi na fedha zote hizi zinatafutwa na Serikali. Kwa hiyo, niombe kuwe na *coordination* kati ya *TANESCO* kwenye kusimamia miradi yote iwe ni ya *MCC*, iwe ni ya *REA* kwa sababu mwisho wa siku *TANESCO* ndiyo watasimamia *maintenance* ya miradi hii yote.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Tumetumia muda mwingi kufanya kazi hii na kila kitu kinaenda kwa ratiba yake, sasa hivi ninaomba kutambua wageni ambao wapo.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dodoma, ninaomba wasimame walipo, ni wanafunzi kutoka *CBE*, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni watano kutoka Chama cha Watabibu wa Dawa Asilia Tanzania, wako wapi hawa jamaa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wawakilishi wa Chama cha Vijana Wasio na Ajira Nchini kutoka Dar es Salaam ambao ni Ndugu Nicholas D. Chihuho na Ndugu Renatus Katondo, karibuni wageni wetu na Mawaziri wenu wako hapahapa, asante sana na mtapata ajira msijibatize namna hiyo msije mkakosa ajira kabisa maana mtu ukimwita jina baya inakuwa hivyohivyo, kwa hiyo jiiteni majina mazuri tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mchungaji Atilio Kilatu wa Kanisa la *Assemblies of God* kutoka Mbeya amemwakilisha Askofu Dkt. Mwaisabila, yupo wapi Mchungaji, ahsante karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mustapha Akunaay ambaye ni Ndugu Ernest J., *I hope I pronounced correctly*. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Rachel Mashishanga ambaye ni Ndugu Pascal Paulo Ndui, yupo wapi? Ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Sabreena Sungura wakiongozwa na Ndugu Omary Hindi, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa CHADEMA toka Mkoa wa Kigoma, naomba Ndugu Omary asimame na wageni wengine waliokuwa pamoja naye wasimame wapo wapi? Naona wamekosa nafasi. *(Makofi)*

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Paul Lwanji, ambaye ni Ndugu Sebastian Kingu kutoka *TMS,* Dar es Salaam, naomba usimame mahali ulipo, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ambao ni Wajumbe 10 wa Muungano wa Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI, Mkuranga (MWAVIUM), naomba wasimame mahali walipo. Ahsante sana, tunapenda kuwapongeza sana na tunasema muishi kwa matumaini na hakuna shaka, siku hizi watu wanaishi miaka mingi kuliko hata watu ambao hawaumwi.

Waheshimiwa Wabunge kuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Masele, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, ambao ni wanafunzi 26 kutoka Chuo cha Madini, Dodoma, wapo wapi wanafunzi hawa? Ahsante sana, karibuni sana. Hiyo ndiyo teknolojia tunaihitaji sasa hivi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Dkt. Titus Kamani, ambao ni Wanachuo wanane kutoka Chuo cha Mipango, Dodoma wakiongozwa na Ndugu Stephano Shola, karibuni sana, naomba msome kwa bidii. *(Makofi)*

Tunao Wageni wa Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, ambao ni Mheshimiwa Sisco Mgeni, Diwani wa CCM, Kata ya Kinyeto, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, karibu Mheshimiwa Diwani.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 18 wa Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakiongozwa na Mstahiki Meya wa Temeke Mheshimiwa Suleiman Hoja, wapo wapi? Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. Nawashukuru kwa kuja na wageni wengine wote mliopo ukumbini mnakaribishwa pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi; kwanza kabisa Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo watakutana katika Ukumbi wa Msekwa 'B' baada ya kuahirishwa shughuli hizi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba watakutana leo hii katika ukumbi Na. 231 baada ya kuahirisha kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii kutakuwa na Kamati Ukumbi wa Pius Msekwa baada ya kuahirisha shughuli hii ya Bunge sasa hivi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo baada ya kuahirisha kikao hiki watakuwa na kazi Ukumbi Na. 227.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Mussa Zungu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao chumba Na. 219, mara baada ya kuahirisha kikao hiki cha Bunge. Mkigongana huko katika hivyo vyumba mtajua wenyewe.

Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Meja Gen. Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo baada ya kuahirisha kikao hiki watakuwa na kikao chao chumba Na. 227.

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Mkoa wa Mbeya kukutana na Mchungaji Atilio Kilatu mara baada ya kipindi cha maswali hapo nje ya ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa David Silinde Katibu wa Chama cha CHADEMA Bungeni, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba, leo baada ya kuahirishwa kwa Bunge kutakuwa na kikao kwenye Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa hiyo wote mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo naomba nieleze yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, tangu tarehe 30 Januari, 2013 hadi jana tarehe 4 Februari, 2013 tuliamua kuwasilisha Bungeni hoja binafsi za Wabunge ambazo ziliahirishwa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge kwa nia njema ili tuweze

kujadili masuala makubwa ya Kitaifa na kuishauri Serikali nini kifanyike ili kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayowahusu wananchi.

Tulikuwa na shughuli nyingine za Serikali, kwa hiyo, zile hoja zote zilizokuwa zimewasilishwa Bunge lile tukaamua kwamba zifike katika Bunge hili. Hata hivyo, imelazimu kuahirisha mijadala ya hoja binafsi kutokana na tabia iliyojitokeza ya utovu wa nidhamu kwa baadhi ya Wabunge na hivyo kuamua kwa makusudi kuanzisha vurugu na hivyo kulifanya Bunge lianze kupoteza heshima yake ya Kibunge mbele ya macho ya Watanzania. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, siku zote nimekuwa nikisisitiza matumizi ya Kanuni za Bunge ambazo ndizo mwongozo wa uendeshaji wa Bunge. Hoja binafsi za Wabunge zinazoongozwa na Kanuni za Bunge kuanzia Kanuni ya 53 hadi Kanuni ya 58 na Kanuni za majadiliano zinazoongozwa na Kanuni kuanzia Kanuni ya 59 hadi Kanuni ya 71 ambazo kwa ujumla wake zikifuatwa kama inavyotakiwa vurugu haiwezi kutokea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano huu imeonesha wazi baadhi ya Wabunge kwa makusudi na kwa nia ya kupotosha wananchi, wakitumia vibaya Kanuni hizi na wakati mwingine kuwadanganya wananchi ambao kwa bahati mbaya Kanuni hizi hawazifahamu.

**MBUNGE FULANI:** Hamna!

**SPIKA:** Ama, Kanuni hazifuatwi na Kiti au zinakiukwa, natoa mifano michache kwa yote yanayojitokeza katika hoja hizi ambazo zimejadiliwa, utii ni bora kuliko sadaka.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa uendeshaji wa hoja binafsi, Kanuni za Bunge zinaeleza wazi kuwa, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja Bungeni ili kupendekeza jambo lolote lijadiliwe, pendekezo hilo linatakiwa liwe limekamilika ili lipate uamuzi bayana wa Bunge kwa kufuata Kanuni ya 54(1) – (2).

Kama hoja inayohusika ni hoja ya Serikali, Msemaji wa Kambi ya Upinzani atapewa nafasi ya kutoa maoni juu ya hoja hiyo na kama hoja inayohusika siyo ya Serikali, Msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni ya Shughuli za Serikali juu ya hoja hiyo, ipo katika Kanuni ya 53(6) (C).

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hapa ilitokea maelezo kwamba upande mwingine ulipaswa usiseme, kwa hiyo, ipo Kanuni kabisa inasema iwapo hoja ni ya Serikali Mwenyekiti na Kambi ya Upinzani wataitolea maoni, iwapo hoja siyo ya Serikali ni ya Mbunge yeyote, upande wa Serikali utatoa maoni.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshuhudia Mbunge analazimisha na kuhoji mamlaka ya Spika kutoa nafasi kwa Mawaziri kuzungumza mara baada ya mtoa hoja na kuonesha kwamba hilo ni kosa, hivyo kuonesha Umma wa Watanzania Kiti kinapendelea. Kwa mujibu ya masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 53(6)(c) ya Bunge imeweka bayana utaratibu utakaotumika kwenye hoja hizi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba, kama hoja inayohusika siyo ya Serikali Msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni ya shughuli za Serikali juu ya hoja hiyo. Kanuni ya 62 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka bayana utaratibu utakaotumika kwenye hoja hizi kwamba kama hoja inayohusika siyo ya Serikali, Msemaji wa Serikali atapewa nafasi ya kutoa maoni ya shughuli za Serikali juu ya hoja hiyo. Kanuni ya 62 ya Kanuni za Bunge imebainisha muda utakaotumiwa na waongeaji kwamba anayetoa hoja anazo dakika 30 na anayetoa maoni ya upande wa pili anapewa muda wa dakika thelathini, Kanuni ya 62. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Spika hataruhusu hoja yeyote inayokiuka Katiba au Sheria au Kanuni za Bunge na Katibu atairudisha hoja hiyo pamoja na vielelezo vyake vyote kwa Mbunge husika na maelezo ya sababu za kukataliwa kwa hoja hiyo, hii ipo katika Kanuni ya 55(9). Iwapo Mbunge anapenda kufanya mabadiliko ya maneno aliyotumia katika hoja anayokusudia kuitoa, anaweza kufanya hivyo kwa kutoa taarifa ya kufanya mabadiliko kabla au wakati wa kuwasilisha hoja yake, hii ipo katika Kanuni ya 55(10) – (11).

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuwa taarifa ya kutaka kufanya marekebisho au mabadiliko itakuwa imetolewa, marekebisho ama mabadiliko yeyote hayatakubaliwa kama kwa maoni ya Spika yataonekana kubadilisha mambo ya msingi yaliyomo katika hoja au yanabadili makusudio au upeo wa hoja hiyo, hii ipo katika Kanuni ya 55(12).

Waheshimiwa Wabunge, hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa; (a) Kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine, (b) Kuondoa maneno fulani bila kuongeza maneno mengine au (c) Kuingiza au kuongeza maneno mapya, hii ni Kanuni ya 57(1).

Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa maneno fulani au kuingiza maneno mengine, basi mjadala juu ya suala la kufanya mabadiliko unaweza kuangalia kwa pamoja yale maneno yaliyopendekezwa, yanayoondolewa na maneno ambayo yanapendekezwa yaingizwe, hii ipo katika Kanuni ya 57(5).

Iwapo hoja inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno, mjadala utahusu tu uondoaji au uingizaji wa maneno mapya kadri itakavyokuwa na hoja hiyo itajadiliwa na kuamuliwa kabla ya ile hoja ya kwanza ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi na hii ipo katika Kanuni ya 57(6) – (7).

Waheshimiwa Wabunge, endapo Spika atasimama wakati Waziri au Mbunge anatoa hotuba Bungeni au atakuwa amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, Waziri au Mbunge huyo ataketi mahali pake na Bunge litabaki kimya ili Spika aweze kutoa maelezo au taarifa yake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hoja ambayo imefanya tufikie maamuzi haya ilikuwa ya jana ya Mheshimiwa Mnyika. Kulingana na maelezo haya ya utangulizi, hoja ya

Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge wa Jimbo la Ubungo, ilikidhi vigezo na ilipewa nafasi ya kuiwasilisha Bungeni na akawasilisha hoja yake.

Baada ya hoja hiyo kuwasilishwa na kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c), Waziri wa Maji ambaye ndiye Msemaji wa Serikali kuhusu maudhui ya hoja husika alipewa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza na kutoa maoni ya shughuli za Serikali juu ya hoja ya Mheshimiwa John Mnyika.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, maoni haya ya Waziri wa Maji yalizingatia Kanuni 57(1) (c), inayohusu kuingiza au kuongeza maneno mapya kwenye hoja iliyotolewa. Kimsingi, Waziri wa Maji aliongeza maneno katika Azimio jipya lililoomba hoja ya msingi iondolewe kwa sababu alizozieleza Waziri.

Hata hivyo, kwa kuwa Kanuni za Bunge haziweki ufafanuzi wa maneno gani yatumike katika kuongeza au kupunguza maneno mapya katika kuifanyia mabadiliko hoja iliyowasilishwa. Hivyo maneno yaliyoongezwa na Waziri ya kuondoa hoja hiyo yalikuwa sahihi na yalikidhi matakwa ya Kanuni za Bunge, kwa kuwa yalikuwa ni sehemu ya maazimio ya hoja yenyewe ambayo iliamuliwa na Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 57(6) – (7) inayotaka hoja ya kuingiza au kuongeza maneno iamuliwe kwanza kabla ya kuendelea na hoja ya awali.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 58 ya Kanuni za Bunge, imeweka masharti ya namna ya kushughulikia mapendekezo ya mabadiliko yote kwenye hoja ya msingi

na Spika amepewa mamlaka ya kuamua mpangilio atakaouona unafaa ikiwa ni pamoja na hoja ya awali.

Waheshimiwa Wabunge Kanuni ya 58 ya Kanuni za Bunge imeweka masharti ya namna ya kushughulikia mapendekezo ya mabadiliko yote kwenye hoja ya msingi na Spika amepewa mamlaka ya kuamua mpangilio atakaouona unafaa ikiwa ni pamoja na kuzingatia masharti yaliyomo kwenye Kanuni ya 53(6)(c).

Katika hoja ya Mheshimiwa Mnyika, ofisi ilipokea mabadiliko manne ambayo yaliwasilishwa na Wabunge, hivyo utaratibu wa Kanuni ungefuatwa kama vurugu zisingejitokeza.

Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa sote tulishuhudia vurugu zilizojitokeza katika Bunge hili hasa wakati wa mjadala wa hoja binafsi za Wabunge, kimsingi huu ulikuwa ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu kutokea katika historia ya Bunge letu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, taasisi ya Bunge inalaani vitendo vilivyojitokeza jana vilivyovunja Kanuni ya 62(2) inayokataza Mbunge kuzungumza kabla ya kuruhusiwa na Spika na Kanuni ya 62(12) inayowataka Wabunge kukaa chini wakati wowote Spika anaposimama kutaka kuzungumza. Aidha, kumekuwa na madai kuwa Kiti kinatoa upendeleo wa wazi kwa Serikali dhidi ya Upinzani, jambo ambalo si kweli. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hivyo basi, kama maamuzi yanayofanywa na kiti yana kasoro Kanuni zinaruhusu Mbunge ambaye hakuridhika na maamuzi hayo kukata rufaa kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge kwa mujibu ...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Kama mnavyo-*misbehave* sasa hivi; kwa kukata rufaa kwenye Kamati ya Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 5(4). Hivyo, vitendo vya uvunjaji wa Kanuni na kusababisha fujo tumedhalilisha Kiti na Taasisi ya Bunge kwa ujumla. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, katika kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi kilichokaa jana, Wajumbe walitafakari kwa undani vurugu hizo zilizojitokeza na kufikia maamuzi yafuatayo:-

Kwanza, Kamati ilikemea kwa nguvu zote vitendo hivyo na kubainisha kwamba endapo vitaachiwa viendelee vinaweza kusababisha madhara makubwa katika ukumbi wa Bunge na nje ya ukumbi wa Bunge. (*Makofi*)

Pili, Kamati ilikubaliana kwamba, suala hili lipelekwe kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ili lichunguzwe na kuleta mapendekezo Bungeni kabla ya Mkutano huu wa Kumi kumalizika.

Tatu, Kamati ilikubaliana kuwa, Hoja zote Binafsi za Wabunge zisiwasilishwe Bungeni kutokana na utovu wa nidhamu uliokuwa umeanza ili kuzuia mwendelezo ambao

ungeweza kujitokeza katika hoja binafsi zilizobaki kwa kulinda heshima ya Bunge.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Kwa hiyo na sisi tunaweza kwa Mujibu wa Kifungu, kuwataja, Mheshimiwa Tundu Lissu, amekuwa kiongozi wa fujo za hapa ndani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lazima tufike mahali tukubali kwamba sisi ni wachaguliwa wa watu. Vitendo vyote vinavyofanyika hapa Bungeni, havilingani na wale waliotuchagua.

Naishukuru sana *TBC* kwa kuonesha kila mtu anayerukaruka na kufanya maneno yasiyo na maana.

Kwa hiyo, naipongeza *TBC* na ikiwezekana, Serikali mjaribu kuipa *TBC* fedha za kutosha waweze kurekebisha mitambo yao. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Ili wote na vitendo vyetu tuweze kuonekana!

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hapa ndiyo mwisho wa matangazo yangu, mwisho wa maelezo yangu na ninasema Kamati ya nidhamu itakaa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Tulieni! Kwanza mmojawapo ni nani? Mheshimiwa Nassari na yeye huwa hajui Kanuni.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Ndiyo!

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, napenda kusema sasa ninalo Tangazo moja la Mwenyekiti wa Kamati ya FEdha na Uchumi - Mheshimiwa Chenge, anataka niwatangazie Wajumbe wake kuwa leo pia watakuwa na Kikao cha Kamati ya Wadau, kwa ajili ya kupitia ule Muswada wa *Miscellaneous Amendment,* na Kikao kitafanyika baada ya kuahirisha Kikao hiki.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Hamwezi kuwa na Mwongozo zaidi ya mmoja. Ni mwongozo mmoja tu, *full stop.* Mheshimiwa Nassari?

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassari.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba Mwongozo wako. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7), pamoja na kwamba umeniambia sijui Kanuni, lakini ninaifahamu Kanuni ya 68 (7) na ninaomba niisome kwako kwa kukuthibitishia kwamba ninaifahamu.

Mheshimiwa Spika, “Halikadhalika Mbunge, anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika, atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge, na majibu ya Spika, yatatolewa papo hapo au baadaye, kadiri atakavyoona inafaa.”

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile niende kwenye Kanuni ya 8 (1), “Kwa kuzingatia matakwa ya Masharti yaliyowekwa na Kiapo cha Kazi yake na kwa madhumuni ya utoaji wa maamuzi, uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa haki na bila upendeleo, Spika, ataendesha Shughuli za Bunge na kutoa maamuzi kwa haki, uadilifu na bila chuki wala upendeleo wowote kwa kuongozwa na Katiba, Sheria za Nchi, Kanuni hizi, Kanuni nyingine zilizopo, Maamuzi ya Maspika wa Bunge waliotangulia na pia kwa kuzingatia Uzoefu pamoja na Mila na Desturi za Mabunge mengine yanayofuata utaratibu wa Kibunge unaofanana na unaofutwa na Bunge la Tanzania.”

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Kanuni ya 58 inayohusu mabadiliko ya hoja na kuondoa hoja, Kanuni ya 58 (5): “Endapo hoja imefikishwa Bungeni, Mtoa Hoja anaweza tu kuiondoa hoja yake kwa kusimama mahali pake na kusema ninaomba ruhusa ya kuondoa hoja. Na papohapo Spika ataliuliza Bunge, kama linaafiki hoja hiyo kuondolewa. Na inapotokea Wabunge walio wengi hawakubali, Spika atasema hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge na Hoja hiyo itakuwa imeondolewa, na Bunge litaendelea na shughuli inayofuata.”

Mheshimiwa Spika, ya mwisho, halafu nitazungumza, ni Kanuni ya 76.

**SPIKA:** Kama umeomba Mwongozo, utanieleza unataka nikuongoze nini?

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana. Kuna Taratibu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nasoma Kanuni ili unipe Mwongozo.

**SPIKA:** Umeomba Mwongozo, sasa usinihutubie, unataka nikwambie nini? *(Kicheko)*

Ndiyo Mwongozo unavyotaka! Ndiyo Mwongozo unavyotaka! Sio kuhutubia watu!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, namalizia Kanuni, halafu niombe Mwongozo, kwa sababu, Mwongozo unaombwa kwa mujibu wa Kanuni hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 76 (1), "Kwa madhumuni ya kudhibiti fujo, endapo itatokea ndani ya Ukumbi wa Bunge na Spika ataona kuwa kuna haja ya kutumia nguvu, basi anaweza kuahirisha shughuli za Bunge bila ya Hoja yoyote kutolewa au kusitisha Kikao kwa muda atakaotaja ili fujo iweze kudhibitiwa na Mpambe wa Bunge." Na (2), "Baada ya utulivu kurudia, Spika atalipeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge." Niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, kwenye ratiba ya Mkutano huu kulikuwa kuna Hoja Binafsi za Wabunge, ikiwemo na hoja yangu ambayo ilipangwa kuwepo mwaka 2012, lakini ikahamishiwa mwaka 2013. Lakini leo tumekuja hapa asubuhi kwenye *Order Paper,* hoja yangu imeondolewa na haipo, wakati Hoja ilishapitia taratibu zote na kukidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, kwa ile Kanuni ya (8) niliyoisoma kwamba, Kiti cha Spika, hususan siku ya jana, kilionesha kuyumba waziwazi kabisa; kwa sababu, Kiti cha Spika kwa mfano, Mheshimiwa Naibu Spika aliniambia mimi nimeingia huku juzi juzi tu na wakati na mimi nimeingia kwa kura za wananchi; na baada ya mimi wameingia na Wabunge wengine, wamepewa na Uwaziri, akina Profesa Mhongo na akina Mbene na wengine, lakini wao hawaonekani kama wameingia juzi humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na vilevile kwamba hoja inapokuja Mezani kwa Kanuni ya 58 niliyoisoma, anayeweza kuiondoa hoja ni Mbunge aliyeleta hoja, ndiye mwenye uwezo wa kuiondoa hoja, na ataiondoa hoja kwa kusema kwamba, anaomba kuondoa hoja na Bunge litahojiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja yangu imeondolewa wakati sijaomba hoja yangu kuondolewa na Bunge halijahojiwa ili kusema endapo linaridhia hoja yangu kuondolewa au isiondolewe. Hoja yangu imeondolewa na Kikao cha Kamati ya Uongozi na wakati Kamati ya Uongozi kazi yake ni kupanga Ratiba ya Shughuli za Bunge peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama fujo zimetokea Bungeni na kusababisha hoja yangu kuamuliwa kuondolewa. Kamati iliyopaswa kukaa kuzungumza ni Kamati ya Maadili, siyo Kamati ya Uongozi! Kamati ya Uongozi kimsingi haina mamlaka ya kuondoa hoja yangu kwenye ratiba ya shughuli za leo na hivyo, ninasubiri Kamati ya Maadili pengine iitishwe wakati nikiwa nimeshawasilisha hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Wananchi wangu wa Arumeru wamejiandaa sana kumwona kijana wao mpendwa waliyempigania mwaka 2012a mwezi wa Nne, kwa nguvu zote, akiwasilisha Hoja Binafsi leo kwa sababu ndio kazi ya Mbunge. Sasa cha ajabu, ninanyimwa kuifanya kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kujua kwamba ni kwa nini nisiwasilishe moja yangu leo? Kwa sababu ilishakidhi vigezo vyote na fujo za jana hazihusiani kabisa na hoja yangu ya siku ya leo. Hoja yangu ya leo ni tofauti ambayo inahusu mwenendo wa Baraza la Mitihani Nchini lilivyoathiri elimu yetu. Hoja yangu haizungumzii vurugu za jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Yote uliyosema ni mema, lakini la msingi ni moja tu. Kamati ya Uongozi ndiyo yenye wajibu wa kupanga ratiba za kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nassari! Aah, sio Mheshimiwa Nassari; wewe Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Katika maelezo yako, umesema, pamoja na mambo mengi mengine kwamba, kwa Taratibu za Kanuni za Bunge, Mbunge ambaye haridhiki na uamuzi wa Spika, anatakiwa akate rufaa.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Rufaa zaidi ya 10 ambazo zimekatwa dhidi ya maamuzi ya kwako wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika dhidi ya maamuzi ambayo mmeyatoa, za tangu mwaka 2011, za mwaka 2012, zitaamuliwa lini? Ni lini utaitisha Kikao cha Kamati ya Kanuni ili isikilize hizo rufaa ambazo mmekatiwa dhidi ya maamuzi ambayo Kiti kimeyafanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mpaka sasa hivi Kamati ya Kanuni haijakaa, haijaitishwa kwa sababu wewe ndiye unayetakiwa kuitisha Kikao hicho, huitishi kwa sababu hutaki maamuzi yako yajadiliwe, tutafuataje? Kiti hakifuati Kanuni! Kama Kiti kinataka Kanuni zifuatwe, rufaa ambazo umekatiwa wewe Mheshimiwa Spika, zisikilizwe ili tujue kama maamuzi unayoyafanya, kweli ni kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba utuongoze hapa, rufaa zetu zitasikilizwa lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwanza, rufaa zote zinafanyiwa kazi. Huwezi kujibu kitu ambacho unafanyia kazi! *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Lakini kwa suala hili hakuna rufaa yoyote iliyokatwa.

Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 57 (1) (c) na Kanuni ya 58 (4).

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yako umesema kwamba, Mheshimiwa Waziri alizungumza jana akichangia kwa kutumia Kanuni ya 53 (6) (c), kama upande wa Serikali unatoa majibu baada ya hoja.

Mheshimiwa Spika, lakini pengine kwa sababu hukuwepo jana, nyaraka ambayo Waziri wa Maji aliiwasilisha na maelezo ambayo aliyatoa Bungeni, kwa ushahidi wa kielelezo hiki, hakutumia kabisa Kanuni ya 53 (6) (c). Kwa hiyo, alichokuwa anakizungumza pale hakuwa anatoa majibu au anachangia hoja, bali kwa mujibu wa nyaraka na ushahidi tulionao, alichokuwa anakifanya yeye na inaanza, Mheshimiwa Waziri wa Maji anasema hivi: “Kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kanuni ya 57 (1) (c).”

Mheshimiwa Spika, Kanuni hiyo inahusu kufanya mabadiliko kwenye hoja. Kwa hiyo, hakuchangia hoja, alianza moja kwa moja kufanya mabadiliko ya kutoa hoja

ya kuiondoa hoja yangu na mwisho akahitimisha, amesaini yeye mwenyewe, akahitimisha na maneno mwisho "naomba kutoa hoja."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo alichokifanya jana, hakuwa anachangia, alitoa hoja ya kuondoa hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni niliyoitaja ya 58 (4), anaeleza kuondoa hoja. Kwa mujibu wa Kanuni ya 58 (4): "Hoja yoyote inaweza kuondolewa wakati wowote kabla ya hoja hiyo kuamuliwa Bungeni iwapo Mbunge mtoa hoja atatoa Taarifa ya Maandishi kwa Katibu wa Bunge ya kuiondoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Kwa kuwa, umesema Bunge hili linaendeshwa kwa Kanuni, na ni wazi Waziri alikiuka Kanuni jana, naomba mwongozo wako, ni hatua zipi ambazo mimi kama Mbunge mtoa hoja naweza kuzichukua kwa Waziri kukiuka Kanuni za Bunge? Zaidi, Waziri kwa kukiuka Kanuni za Bunge, kwa hoja yake aliyoitoa alitumia maelezo potofu ya kutaja miradi ambayo haijatengewa pesa kwenye bajeti akajenga picha kwamba Dar es Salaam tayari ina pesa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninao ushahidi wa nyaraka za Waziri mwenyewe, Kauli ya Serikali aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 07 Novemb,a 2012, Randama ya Wizara na Nyaraka nyingine mbalimbali ambazo zinaonesha Waziri alilipotosha Bunge kwenye maelezo aliyoyatoa jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako wa hatua za kuchukua za kumwajibisha Waziri, kwa kukiuka

Kanuni za Bunge na kwa kutoa maelezo potofu Bungeni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kanuni za Bunge, hazikuvunjwa kwa sababu…

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Ndiyo! Kwa sababu, Kanuni ya 53 (6) (c) imetoa utaratibu wa namna ya kutumia muda.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Kwa hiyo, huwezi kusimama na ku…

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Nataka Utaratibu. Kanuni ya 53, huwezi kusema kila mtu na mimi Spika, naomba kutumia dakika 15 kuzungumza, haiwezekani! Alichangia kwa kufanya mabadiliko kwa kutumia Kanuni ya 57.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**SPIKA:** Sasa, hoja yako ya kwamba Waziri amelidanganya Bunge, unatafuta utaratibu mwingine wa kuwasilisha hoja namna hiyo. Lakini kwamba jana alivunja Utaratibu, siyo kweli.

Tunaendelea. Wote wamemalizika! Mheshimiwa Machemli!

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47, naomba niisome. "Baada ya muda wa Maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa Shughuli za Bunge, kama zilivyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea sasa hivi, Askari wa Kenya, Askari wa Uganda wamevuka mipaka ya nchi yao, wameingia Tanzania katika Jimbo langu la Ukerewe, katika Wilaya ya Ukerewe, wanafanya shughuli za Kijeshi. Wanapiga wananchi, wanawadhalilisha, wanawaumiza kwa kisingizio cha kusaka nyavu haramu.

Mheshimiwa Spika, amani imetoweka katika nchi yetu. Sasa ningeomba Bunge lako lijadili suala hili kwa sababu ni uvunjifu wa amani na askari wale kutoka nchi ya jirani wameingia kwetu na kuvuka mipaka ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. *(Kicheko)*

Sasa naagiza, Serikali kesho itoe maelezo ya suala hili. Hatuwezi kujadili kitu ambacho hatukifahamu. Serikali kesho watatoa maelezo ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla! Dkt. Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, toka niingie hapa Bungeni nimekuwa nikishuhudia vitendo vingi sana vya kupoteza *insights* miongoni mwa Wabunge. Sasa nilikuwa naomba kupata Taarifa kama Ofisi yako inaweza ikatenga Ofisi Maalum ambapo itakuwa ikitoa huduma za kutibu Wabunge ambao wana matatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MBUNGE FULANI:** Taahira. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MBUNGE FULANI:** Wape dozi hao. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Tunao utaratibu. Upo utaratibu! Tuna Zahanati, kama Wabunge wana homa, wanakwenda kutibiwa kule. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona sasa tunaendelea kupoteza muda. Napenda kusema kwamba, Kamati zote ambazo ziliomba kufanya kazi, wafanye kazi baada ya kipindi hiki.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

*(Saa 5.35 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarahe 6 Februari, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*